**Arise** B.V Uholanzi yaingia ubia hisa mil. 174 na NMB

UKURASA 2



**Viongozi** wa umma 187 kikaangoni kutorejesha tamko rasilimali, madeni

UKURASA 3


# Nipashe

Ijumaa Januari 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580454

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Guardiola amwaga sifa kwa Stones**

UKURASA 21

# Kiama watiririshaji majitaka chawadia

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**JAFO ASHTUKIA WIZI MAMILIONI**
WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa...

UKURASA WA 4
**MWANAFUNZI ANAYEDAIWA KUTOROSHWA APATIKANA**
MWANAFUNZI wa kike wa shule ya sekondari (jina linahifadhiwa)...


## Polisi 4 wafukuzwa kazi madai ya rushwa na uhalifu

UKURASA 3



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakifanya maandalizi ya kununua vifaa vya shule kwa ajili ya watoto wanaotarajiwa kufungua shule hivi karibuni, katika mitaa ya Kariakoo, jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**


Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


# Watumishi matatani tuhuma kulipana posho fedha za JPM

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA KUJIULIZA Z'BAR** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## Arise B.V yaingia ubia hisa milioni 174 na benki NMB

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Masoko ya Mitaji na Dhamana nchini imeidhinisha uhamishaji wa jumla ya hisa 174,500,000 zilizokuwa benki ya NMB kutoka Rabobank kwenda taasisi ya fedha Arise ya nchini Uholanzi.

Uhamishaji wa hisa hizo ulikamilika rasmi Desemba 31, mwaka jana.

Taarifa iliyotolewa na Arise kwa vyombo vya habari jana, ilisema taasisi hiyo inamiliki asilimia 34.9 ya hisa za NMB ambazo zimeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salam.

Ilisema hisa hizo zilikuwa zinamilikiwa na Rabobank ambayo ni mshirika wa Arise. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Arise, Deepak Malik, alisema kukamilika kwa uhamishaji hisa ni hatua muhimu kwa taasisi hiyo.

"Lengo kuu la Arise ni kuingia ubia na taasisi endelevu za kifedha za ndani, ili kuongeza nguvu na kukuza upatikanaji wa huduma za kifedha zenye ufanisi na jumuishi barani Afrika. Hili litasaidia kukuza uchumi na kupunguza umaskini," alisema Malik.

Alisema Arise inaiona Tanzania ni nchi inayofaa kwa uwekezaji katika eneo la Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na kuongeza kuwa ubia kati yake (Arise) na NMB itakuwa na matokeo chanya katika kuongeza upatikanaji wa huduma jumuishi za fedha barani Afrika. Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema kufanikiwa kukamilika kwa uhamisho wa hisa hizo ni uthibitisho tosha wa imani ya wawekezaji katika Benki ya NMB na taifa.

"Ubia huu shirikishi kati ya Arise na NMB unalenga kuleta faida kubwa ambayo itazidi matarajio ya wanahisa wetu katika nyanja za utendaji, biashara, muundo na fedha," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa za fedha za benki za robo ya tatu ya mwaka 2020, NMB inaongoza kwa ukubwa wa thamani za mali Tanzania.

"NMB ni benki kubwa Tanzania kirasilimali kwa mujibu wa taarifa za fedha za robo ya tatu ya mwaka huu. Rasilimali zake ziliongezeka kwa kuweka rekodi hadi kufikia Sh. trilioni 7.0 kutoka Sh. trilioni 6.1 kipindi kama hicho mwaka 2019," alisema.

Alisema benki hiyo pia imepata faida ya Sh. bilioni 145 kipindi cha robo ya tatu ya mwaka ulioishia Septemba 30, 2020, kutoka Sh. bilioni 82 mwaka 2019. "Bila shaka uwekezaji huu wa muda mrefu wa Arise utasaidia matarajio ya ukuaji wa NMB na kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa Tanzania kupitia ongezeko la huduma jumuishi za kifedha na ukuaji wa sekta za biashara ndogo na za kati, kampuni za kijasiriamali na kilimo."

Alisema Arise itasaidia NMB hasa katika kutoa miongozo na ushauri wa uendeshaji wa biashara sambamba na matakwa ya kanuni za kimataifa.

"Ni matumaini yetu kuwa ubia huu utaleta matokeo chanya kwa benki ya NMB na Arise," alisema Malik.

# Kiama chawadia watiririshaji majitaka

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, ameweka wazi kwamba, wanaotiririsha majitaka kiholela, kiama chao kipo njiani.

Amedokeza baadhi ya hatua hizo kali ni kutungwa kwa sheria zitakazowabana wanaokiuka kanuni hizo za afya, sambamba na kuwafuatilia kwa karibu wanaopuuzia elimu itakayotolewa kwa kuendelea kutiririsha uchafu huo ovyo.

"Nimepita Mikocheni, nimekutana na hali hiyo. Sasa, jiulize aina ya watu wanaoishi huko halafu wanashiriki kutiririsha majitaka kuelekeza kwenye mito," aling'aka Kunenge katika hali ya kukereka.

Mkuu wa Mkoa huyo ambaye kabla ya wadhifa wa sasa alikuwa Katibu Tawala wa Dar es Salaam, alitoa kauli hiyo jana alipojibu moja ya maswali aliyoulizwa na waandishi wa habari wa vyombo vya habari vya Kampuni za IPP, alipozuru kwenye makao makuu yake na kuzungumza na wafanyakazi.

Alisema amesikia kilio dhidi ya kadhia hiyo na hatua za awali alizochukua, zinajumuisha kuzifanyia marekebisho baadhi ya sheria na kanuni zake kwa lengo la kuja na adhabu kali zaidi kwa wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Kunenge alisema wamebaini adhabu iliyopo kisheria kwa sasa kwa mtu anayetiwa hatiani kwa kutiririsha majitaka (faini ya Sh. 50,000), ni ndogo kulinganisha na gharama za kuita gari la kunyonya majitaka.

Alisema tayari amezishaagiza manispaa kuzipitia upya sheria hizo ili kuweka adhabu kali zaidi kwa wanaotiririsha majitaka katika mifereji ya barabara na mito jijini.

Kiongozi huyo alisema mifereji iliyopo, iliyojengwa mahususi kupitisha maji ya mvua na siyo kupitisha majitaka, kunakofanywa na baadhi ya wakazi wa jiji hilo.

"Tunawaambia wananchi tunajenga mifereji kwa ajili ya maji ya mvua lakini bahati mbaya sana wanaunganisha majitaka kwenye mifereji ile na tumeona tatizo hilo, lazima tuwe na mabadiliko ya kitabia.

"Sasa hivi, tumeona adhabu ya kutiririsha majitaka ni ndogo kuliko gharama za kukodi gari la kutoa majitaka. Kwa hiyo, nimeshaelekeza manispaa wabadilishe, waongeze adhabu iwe kubwa kuliko gharama ya kukodi gari," alibainisha.

Katika ziara yake hiyo, Kunenge alianika mipango iliyopo kukabiliana na tatizo la utupaji wa taka ovyo, akibainisha mpango unaoendelea wa kuboresha dampo la Pugu na kujenga madampo mengine katika wilaya zote za Dar es Salaam.

Alisema uongozi wa mkoa huo pia unajipanga kuhimili kiwango cha taka kinachozalishwa kwa kujenga kiwanda cha kuchakata taka Mabwepande, taka zikigeuzwa kuwa mbolea.

Alisema kiwanda cha kuchakata taka cha Mabwepande kinatarajiwa kuchakata tani 50 za taka na zitazalisha tani 30 za mbolea kwa siku, hivyo kuwa chanzo mojawapo cha mapato kwa manispaa husika na kupunguza gharama za uzoaji taka kwa wananchi.

Kunenge alisema jitihada za mkoa kuimarisha usafi wa jiji hilo la kibiashara, zinakwamishwa na baadhi ya wananchi wanaondekeza utupaji wa taka ovyo, akitolea mfano wakazi wa Kiwalani wilayani Temeke ambako serikali ilijenga mifereji na kuboresha mazingira ya mto, lakini baada ya muda mfupi, mto na mifereji ikajazwa taka.

Vilevile, Mkuu wa Mkoa alizungumzia hatua za kiserikali kukabiliana na mafuriko eneo la Jangwani, kwamba tayari mchakato wa kujenga daraja lenye urefu wa mita 300 umeanza, mradi ukitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 32.

●**Imeandikwa na Enock Charles na Maulid Mmbaga. Picha Uk. 7**



Mkurugenzi Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI), Dk. Ismael Kimerei (wapili kulia), akimwelezea jambo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, alipotembelea taasisi hiyo, iliyopo jijini Dar es Salaam Januari 6, 2021. Kushoto ni Mratibu wa Mradi wa SWIOFish, Dk. Nichrous Mlalila. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

# Watumishi matatani tuhuma kulipana posho fedha za JPM

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATUMISHI katika Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, wameingia matatani baada ya kudaiwa kulipana posho Sh. milioni 16.177 ambazo ni kati ya Sh. milioni 200 zilizotolewa na Rais John Magufuli kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mnyagala wilayani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alipata taarifa ya kutafunwa fedha hizo baada ya kufanya ziara katika wilaya hiyo kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika wilaya hiyo.

"Inakuwaje hela ambayo Mheshimiwa Rais ametoa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya nyie mnalipana posho, milioni 16 ambazo tungeweza kununulia mashine ya kufyatulia tofali?" Alihoji.

Homera aliagiza watumishi wote waliolipana posho hiyo kufikia Jumatatu wazirejeshe fedha hizo, ili zitumike kuchimba kisima cha maji na kukataa kuweka jiwe la msingi hadi hapo fedha hizo zitakapopatikana.

"Mfano DC (Mkuu wa Wilaya) kila siku anakuja hapa analipwa posho, mkurugenzi ukija kutembelea mradi hapa unalipwa posho... hapana! Sasa inakuweje watu wanaokuja kusimamia hapa wanalipwa posho?" Alihoji.

Awali, Ofisa Mipango Wilaya Tanganyika, Dotto Kwigema, akisoma taarifa ya ujenzi ya kituo hicho cha afya kwa Mkuu wa Mkoa, alisema katika mradi huo, serikali ilitoa Sh. milioni 200 ambapo hadi sasa zimetumika Sh. 200,500,000.

Kwigema alitoa mchanganuo jinsi fedha hizo zilivyotumika kuwa ni Sh. milioni 165.834 zilizotumika kununulia vifaa, Sh. milioni 26.99 malipo ya mafundi na vibarua na ununuzi wa trekta, Sh. 16,177,000 kulipa posho wasimamizi wa mradi na Sh. 500,000 ni nguvu za wananchi.

Katika mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi (stendi), Mkuu wa Mkoa, Homera aliagiza Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Tanganyika na wahandisi kutoa maelezo ni kwanini mradi huo umekwama kwa miezi minne.

Homera alisema serikali inapata aibu kutokana na kutelekezwa kwa ujenzi wa stendi hiyo wakati jitihada kubwa zilifanyika kupata shilingi milioni 75 kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

"Tanganyika ni wilaya nzuri sana, lakini 'the way' inavyokwenda, inakwenda kuharibika, kuna vitu vingine vinakwenda vizuri kama kilimo, lakini ukifika kwenye miradi, Tanganyika ni mzigo, haiwezekani hata mkandarasi hayupo eneo la kazi," alisema.

Mkuu wa Mkoa huyo aliiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na vyombo vingine kuchunguza mradi wa ujenzi wa stendi na ripoti itolewe baada ya siku saba.

# Askari walionaswa tuhuma rushwa, uhalifu wafukuzwa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha limewafukuza kazi askari wanne wanaodaiwa kujihusisha na matukio mawili tofauti ya kihalifu, akiwamo William Joseph, aliyekamatwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Kenani Kihongosi.

Askari Joseph alikutwa na matukio ya kihalifu likiwamo la kujiunganishia umeme kinyume cha sheria, misokoto 20 ya bangi, pombe ya moshi lita tano, vyuma vya bomba vya miradi ya serikali inayoendelea kutekelezwa, mafuta ya dizeli lita 85, pombe ya viroba boksi 84, chupa za konyagi tisa zenye vimiminika ndani na pakiti tatu za pombe aina ya kiroba zikiwa na kimiminika ndani.

Askari wengine waliofukuzwa kazi kwa tuhuma za kushawishi na kupokea rushwa Desemba 24, mwaka jana kutoka kwa mmiliki wa kampuni ya Germs and Rocks Ventures ya jijini Arusha ni Heavenlight Mushi ambaye ni askari polisi Intelijensia Mkoa wa Kinondoni.

Wengine ni Gasper Paul, askari Intelijensia Makao Makuu ya Jeshi hilo na Bryton Murumbe ambaye ni askari Polisi Kazi za kawaida Mkoa wa Dodoma.

Akizungumza jana ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alisema tukio la kwanza la askari Joseph ni kukamatwa na Mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama na Mkuu wa Wilaya ya Arusha Kihongosi, Januari 5, mwaka huu, kati ya majira ya saa 3:00 na saa 5:00 usiku, Mtaa wa Muriet, Kata ya Sokoni One, Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Alisema Kihongosi aliambatana na Mkuu wa Upelelezi wilaya hiyo (OCD) na viongozi wengine wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), baada ya kupata taarifa za siri kuhusu kuwapo kwa mtu anayetumia umeme kinyume cha sheria.

Hamduni alisema baada ya jeshi hilo kukamilisha taratibu za kijeshi na kuwafukuza kazi yeye na wenzake, kuanzia Januari 6, mwaka huu, tayari upelelezi umekamilika na majalada ya kesi zao yamepelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria.

Alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kufichua na kutoa taarifa za wahalifu ili wachukue hatua dhidi yao.

Akielezea tukio la askari watatu waliofukuzwa kazi kwa tuhuma za kujihusisha na kupokea rushwa, alisema askari hao, wakiwa na raia sita (hakuwataja majina yao) walikamatwa Desemba 24, mwaka jana wakishawishi na kupewa rushwa na kampuni hiyo.

Mapema Desemba mwaka jana ilidaiwa na Kamanda Hamduni kuwa askari hao watatu wanadaiwa kumteka mfanyabiashara wa madini jijini Arusha, Sammy Mollel ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Madini ya Germs and Rocks Venture ya jijini humo na kujipatia Sh. milioni 10 kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa askari hao walikamatwa ofisini kwa Mollel Desemba 24, mwaka jana, baada ya kufika kwa mara ya pili ili kuchukua mgao wa pili wa Sh. milioni 20 kati ya Sh. milioni 30 walizohitaji kupatiwa.

# Jafo ashtukia wizi mamilioni

**Na Neema Emmanuel,**
GEREMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameshtukia wizi wa Sh. milioni 350 za makusanyo ya mapato ya ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Yanga Makaga, alisema hayo wakati akizungumza mbele ya Waziri Jafo, aliyekuwa kwenye ziara wilayani humo.

Makaga alisema fedha hizo zimetafunwa na watumishi wa halmashauri hiyo baada ya kuzikusanya kwa kutumia mfumo wa mashine za POSS.

Alisema watumishi hao hawakuziingiza fedha hizo kwenye akaunti ya halmashauri badala yake walizitafuna.

Ubadhirifu huo, umedaiwa kufanyika baada ya Baraza la Madiwani kuvunjwa mwaka jana na baraza jipya lilipoapishwa liliagiza wachukuliwe hatua za kisheria, lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika.

"Mheshimiwa waziri kuna watumishi walitafuna fedha za mapato baada ya kuzikusanya wakitumia mashine za POSS, ubadhirifu huo waliufanya kipindi ambacho baraza la madiwani lilivunjwa na hakuna hatua zilizochukuliwa," alisema Yanga.

Alisema kutochukuliwa hatua watumishi hao kulichangia aliyekuwa mweka hazina wa halmashauri hiyo ambaye alikuwa akituhumiwa kwa upotevu wa fedha Sh. milioni 900, mwaka 2018/2019, kuhamishiwa Wilaya ya Missenyi ndani ya siku tatu baada ya upotevu huo kubainika, licha ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuchunguza na kubaini alikuwa na kesi ya kujibu.

"Huyo mtumishi alihamishwa ndani ya siku tatu baada ya upotevu wa fedha kufahamika, licha ya TAKUKURU kumhusisha na upotevu wa fedha hizo na hakuchuliwa hatua na kwa sasa amestaafu," alidai mwenyekiti huyo wa halmashauri.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Boniface Magesa, alisema watumishi waliohusika na upotevu wa mapato ya POSS baada ya tuhuma hizo, waliandikiwa barua warejeshe fedha hizo na baadhi wamerejesha kidogo.

Kutokana na tuhuma hizo, Jafo alimhoji mkurugenzi huyo sababu za watumishi hao kutochukuliwa hatua na bado wako kazini.

"Nimegundua DED ndiye mwenye matatizo, watumishi kwa nini hawajachuliwa hatua, haiwezekani mtu kachukua fedha halafu yuko kazini, angalieni sheria inasema nini vinginevyo nitaingalia kwa jicho lingine Halmashauri ya Sengerema," alionya Jafo.



# Ukimwona mtoto huyu toa taarifa

**Na Mwandishi Wetu**

MTOTO Queen Seraphine mwenye umri wa miaka mitatu na nusu, anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka katika mazingira ya kutatanisha nyumbani kwao Tabata Shule jijini Dar es Salaam.

Mama mzazi wa mtoto huyo, Rose Monde, alisema jana kuwa mwanawe huyo alitoka nyumbani Januari 6 mwaka huu, majira ya saa tatu asubuhi akiwa na dada yake aitwaye Daines Seraphine walipotumwa kwenda kununua vitafunwa mtaa jirani na nyumbani kwao.

"Inasemakana wakati wakinunua vitafunwa, alifika mama mmoja na kuwaambia eti wamesukwa vizuri, wamependeza, na kumtaka Queen amlete kwangu nimsuke," alidai Monde.

"Kwa mazingira hayo ni wazi kwamba mwanangu ameibwa na nimeshatoa taarifa Kituo cha Polisi Tabata na kufungua jalada namba TBT/RB/104/2021 na ninaomba wasamaria wema wanisaidia kumpata mwanangu," alisema, wawasiliane naye kwa simu namba **0718-500299 ama 0657-397772.**

# Viongozi 187 wa umma kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma imesema itawachukuliwa hatua za kisheria viongozi 187 ambao hawajarejesha matamko yao ya rasilimali na madeni.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Maadili, Jaji Sivangilwa Mwangesi, urejeshaji wa matamko hayo ulikoma Desemba 31 mwaka jana. Jaji Mwangesi alibainisha kuwa, kati ya viongozi wa umma 15,110 wanaowajibika chini ya kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma namba 13 ya mwaka 1995, hadi Desemba 31 mwaka jana, viongozi waliorejesha matamko ni 14,923.

Alisema idadi hiyo ya waliorejesha ni sawa na asilimia 98.8, huku wasiorejesha ni asilimia 1.2. "Viongozi ambao hawajarejesha matamko yao taratibu za kisheria zitafuatwa dhidi yao, pia kwa matamko ya viongozi ambayo tumepokea tutaendelea na uchambuzi kubaini usahihi wa taarifa zilizomo," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.t
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,40470
DODOMA
Tarehe 08/01/2021

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA** tarehe 08-01-2021 kampuni ya HAINAN INTERNATIONAL LTD itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili:

   T 175 DFN / T 168 DFN.

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 2.82 |
| Kimo | - | mita | 5.00 |

3. Njia itakayotumika: **SINGIDA** hadi **DAR ES SALAAM** kupitia **MOROGORO**.

   Gari itasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.



**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**REQUEST FOR PROPOSAL: No. RFP/2020/SUP/049**
**FOR THE PROVISION OF INTERNET SERVICES FOR UNHCR TANZANIA OPERATION**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers to submit firm offers for establishment of the service contract(s) for provision of internet services for UNHCR Tanzania operation.

**2. Eligibility:**

Suppliers duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

**Kindly download the tender documents in the below link:**

**https://drive.google.com/drive/folders/1fmqQdz_M-FKhM8yZK-MA0qex5mU6rMf_V?usp=sharing**

If you fail to access the link, please write to **ishobeza@unhcr.org** copy **ndassa@unhcr.org**

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference meeting will be held | Wednesday 06th January 2021 |
| Deadline for receiving requests for clarification | Wednesday 20th January 2021 at 1700 hrs EAT |
| Deadline for submission of offers | Friday 29th January 2021 at 1700 hrs, EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

## TAARIFA KWA UMMA

### UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU ZA MAHESABU YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI PAMOJA NA KUMBUKUMBU MUHIMU ZA KISHERIA

Kwa mujibu wa **Kifungu cha 89 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148 ("Sheria ya VAT"),** mtu yeyote, kampuni, au Taasisi iliyosajiliwa kama mlipakodi wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) analazimika kisheria kutunza kumbukumbu za mahesabu, nyaraka, marejesho, au nyaraka nyingine zozote zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria ya VAT au Sheria nyingine yeyote inayoambatana nayo.

Kama, **Kifungu cha 89(i)(d) cha Sheria ya VAT** kinamlazimu kila aliyesajiliwa kulipa VAT kutunza kumbukumbu sahihi za **Akaunti ya Kodi ya Ongezeko la Thamani,** yaani, **"Value Added Tax Account",** kumbukumbu za kila kipindi cha mahesabu, malipo yaliyofanyika na mhusika, kodi husika aliyokubaliwa kujirejeshea kutokana na manunuzi pamoja na ongezeko au upungufu katika marekebisho ambayo, mlipakodi husika kafanya au anastahili katika kipindi husika. Aidha, **Kifungu cha 35 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438** kinaruhusu kila mlipakodi kutunza kumbukumbu kwa njia ya karatasi au kielektroniki kwa ajili ya kuwezesha ukadiriaji sahihi wa kodi.

Katika juhudi zetu za usimamizi na ufuatiliaji wa VAT, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tumegundua, kwa masikitiko makubwa, kuwa baadhi ya walipakodi waliosajiliwa kwa VAT hawafuati matakwa haya mahususi ya Sheria, na hasa hitaji la lazima la utunzaji wa mahesabu kwenye **Akaunti ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.** Kitendo hiki, ambacho hakikubaliki hata kidogo, ni hujuma ya wazi inayodhoofisha ukusanyaji wa kodi halali ya Serikali na kuihasibu kwa wakati.

Hivyo, kufuatia ufafanuzi na maelezo mahususi hapo juu, **TAARIFA HII KWA UMMA,** inalenga kuwaasa na kuwakumbusha walipakodi wote nchini (ikijumuisha makampuni, Taasisi, au watu binafsi) waliosajiliwa kulipa VAT, ambao wamekuwa hawafuati Sheria tajwa, kwa utimilifu wake, kufanya hivyo mara moja.

Fahamu kwamba kukosa kutunza hesabu za **Akaunti ya Kodi ya Ongezeko la Thamani,** ikiwa ni pamoja na kumbukumbu nyingine muhimu kwa mujibu wa Sheria, ni uvunjaji wa Sheria na mhusika, endapo atabainika, ataadhibiwa kwa mujibu wa **Kifungu cha 77 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438.**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:-**

**Dr. Edwin P. Mhede, Ph.D.**
**KAMISHNA MKUU**

# Mwanafunzi anayedaiwa kutoroshwa apatikana

**Na Thobias Mwanakatwe**

MWANAFUNZI wa kike wa shule ya sekondari (jina linahifadhiwa), aliyedaiwa kutoroshwa na mfanyabiashara mmoja maarufu wilayani Kyela, mkoani Mbeya, amepatikana ikiwa ni siku tisa tangu atoroshwe.

Mwanafunzi huyo anayesoma kidato cha pili, jana alipelekwa na baba yake mzazi katika Kituo cha Polisi Kyela Mjini kwa ajili ya kutoa maelezo jinsi alivyotoroshwa na mfanyabiashara huyo na kuzua taharuki kwa familia.

Chanzo cha habari kutoka Kituo cha Polisi Kyela Mjini, kililiambia gazeti hili kuwa katika maelezo aliyoyatoa kituoni hapo, alithibitisha kutoroshwa na mfanyabiashara huyo ambaye alikuwa naye siku zote na Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka.

Wazazi wa mwanafunzi huyo walimpeleka katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela kupimwa afya na vipimo vimethibitisha alibakwa.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo (jina linahifadhiwa), alisema mtoto wake aliwasili juzi jioni kwa basi dogo ambalo alipandia eneo la Uyole.

Alisema mwanafunzi huyo alianza safari yake jijini Dar es Salaam ambako alipandishwa basi na mfanyabiashara anayedaiwa kumtorosha.

"Alipandishwa kwenye basi kutokea Dar es Salaam na tiketi amekuja nayo, lakini bahati mbaya basi hilo liliharibika njiani na hivyo kuamua kupanda basi dogo la abiria aina ya coaster," alisema.

Mfanyabiashara huyo anayedaiwa kumtorosha mwanafunzi huyo alishafunguliwa jalada namba KY4IR/07/2021 katika Kituo cha Polisi Kyela.

Baba mzazi wa mwanafunzi huyo, akizungumza na gazeti hili, alisema mtoto wake alitoroshwa na mfanyabiashara huyo Desemba 29, 2020 saa 1:30 usiku na kumpeleka kwenye moja ya hoteli za kitalii.

Alisema Desemba 30, 2020 mfanyabiashara huyo alimtuma rafiki yake wa karibu (jina tunalo) kwenda kuonana na wazazi wa mwanafunzi huyo.

"Rafiki wa mfanyabiashara huyo alipokuja kwangu kuniona alinieleza kuwa ametumwa na mfanyabiashara kwamba tusimtafute yuko naye na kwamba anaomba amuoe kabisa na yuko tayari kutoa hela atakayohitaji," alisema.

Hata hivyo, wazazi walikataa ombi la mfanyabiashara huyo badala yake walimweleza aliyetumwa akamwambie kuwa amrejeshe nyumbani mwanafunzi huyo na baada ya kurudi watampima kuona kama yuko salama.

Tangu Desemba 31, 2020 hadi Januari 4, mwaka huu mfanyabiashara huyo alikuwa hajamrejesha mwanafunzi huyo nyumbani kwao hatua ambayo ilimfanya baba mzazi kwenda kituo cha polisi kutoa taarifa.

# Waziri ataka sababu wamiliki kushindwa kuchukua hati ardhi

**Na Munir Shemweta, TANGA**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi kufanya utafiti sababu zinazowafanya wamiliki wa ardhi kushindwa kujitokeza kuchukua hati za ardhi zilizokamilika.

Dk. Mabula alitoa kauli hiyo jana katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wakati akigawa Hati za Ardhi kwa wakazi wa jiji hilo akiwa katika ziara yake ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ukusanyaji maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Alisema ni lazima watendaji wa sekta ya ardhi nchini kuanza kujiuliza tatizo liko wapi mpaka wamiliki wa ardhi ambao hati zao zimekamilika, wanashindwa kujitokeza kuzichukua katika ofisi za wasajili wa hati wasaidizi kwenye ofisi za ardhi za mikoa.

Kwa mujibu wa Mabula, kati ya wamiliki wa ardhi 80 walioarifiwa kwenda kuchukua hati zao katika Jiji la Tanga, ni wamiliki wanane tu waliojitokeza kuzichukua jambo alisema si sahihi.

Aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi kuwahimiza wamiliki wa ardhi wakati wa kuandaliwa hati kwenda kuchukua kwa wakati sambamba na kuwakumbusha masharti ya umiliki kama vile viwango wanavyotakiwa kulipa kama kodi ya pango la ardhi na kuendeleza kiwanja ndani ya miaka mitatu.

"Ukichukua hati unaongeza thamani ya eneo lako maana usipochukua kunakuwa na masharti mengi wakati wa kutaka kuuza. Eneo la Sh. milioni 20 unaweza kuliuza kwa Sh. milioni tano, huku anayelinunua anaweza kuliuza hata kwa Sh. milioni 200," alisema. Naibu Waziri aliongeza kuwa kwa sasa watendaji wa wizara yake wanafanya kazi kama mchwa ili kuhakikisha mambo wanayopanga yanafanyika kwa mafanikio makubwa.

Mmoja wa wananchi waliopatiwa hati na Naibu Waziri, ambaye alikuwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambaye sasa ni Mbunge wa Katavi, Mhandisi Isack Kamwele, aliipongeza wizara kwa utaratibu iliyouanzisha ya kuwapigia simu wamiliki wa ardhi ambao hati zao zimekamilika.

"Mimi nilipigiwa simu na ofisi ya ardhi mkoa kuelezwa kuwa hati yangu iko tayari. Uamuzi wa kupigiwa simu ni utaratibu mzuri na hii sasa ni dunia ya kwanza na tukiendelea na utaratibu huu, malalamiko yatapungua sana. Ila naomba muongeze kasi katika utoaji vibali vya ujenzi," alisema.

# MATANGAZO

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF WATER

### REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)

COUNTRY: **Tanzania**

Name of Project: **Second Water Sector Support Project (WSSP II)**
Credit No: **59490**
Project ID No: **P150361**
Assignment Title: **Consultancy Services for Review and Up-Date of the Detailed Engineering Designs and construction Supervision of the Proposed Wastewater Infrastructure for Tanga City**

Tender No.**ME-011/2020-2021/C/18**

Reference No.**TZ-MOW-195742-CS-CQS**

1. This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for the project that appeared in the United Nations Development Business; Issue No. WB5803 – 12/16 of December 21, 2016.

2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank towards the cost of the Water Sector Support Project (WSSP II) which is part of the Second Water Sector Development Program (WSDP II), and intends to apply part of the proceeds for consulting services.

3. The consulting services ("the services") include Provision of Consultancy Services for Review and Up-Date of the Detailed Engineering Designs and construction Supervision of the Proposed Wastewater Infrastructure for Tanga City. The assignment includes Review and update of the designs, preparation of the Tender Documents, Supervision of construction of the wastewater treatment plant, sewerage network and sewage pumping stations. The assignment will be undertaken in a period of 30 months exclusive of the Defect Liability Period which will be 12 months.

4. The Ministry of Water (MoW) now invites eligible consultants to express their interest in providing the services. Interested Consultants should provide information indicating that they are qualified to perform the services. The short listing criteria are:(i) core business of the firm and the number of years in business;(ii) experience in similar assignment (Detailed Engineering Design and construction Supervision preferably Water Projects) (iii) experience of having worked in sub-Saharan Africa or similar environment;(iv) technical and managerial capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff. Do not provide CV's of staff since key experts will not be evaluated at the short-listing stage).Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a sub consultancy to enhance their qualifications.

5. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the World Bank's Guidelines: Selection and Employment of Consultants [under IBRD Loans and IDA Credits & Grants] by World Bank Borrowers, January 2011, revised July 2014 ("Consultant Guidelines"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

6. A Consulting Firm will be selected in accordance with the Consultant Qualification Selection (CQS) Method set out in the World Bank Guidelines.

7. Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 8:00 to 15:30 hours, Monday to Fridays inclusive, except on public holidays.

8. Expression of Interest marked **"EXPRESSION OF INTEREST PROVISION OF CONSULTANCY SERVICES FOR REVIEW AND UP-DATE OF THE DETAILED ENGINEERING DESIGNS AND CONSTRUCTION SUPERVISION OF THE PROPOSED WASTEWATER INFRASTRUCTURE FOR TANGA CITY"** should be delivered in a written form to the address below (in person, or by courier, or by e-mail) by 27th January 2021 at 14:00 hour's local time.

Physical Address:
The Secretary Ministerial Tender Board
Ministry of Water,
Kolon Building adjacent to DUWASA Head Office, PMU Offices,
Chimwaga Road,
40473 Dodoma, Tanzania

Attention:
Dr. Christopher P. Nditi
Director of Procurement Management Unit
Telephone: **+255 716 308473**
E-mail: pmu@maji.go.tz

**PERMANENT SECRETARY**
**MINISTRY OF WATER**

## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF WATER

### REQUEST FOR EXPRESSIONS OF INTEREST (CONSULTING SERVICES – FIRMS SELECTION)

COUNTRY: **Tanzania**

Name of Project: **Second Water Sector Support Project (WSSP II)**
Credit No: **59490**
Project ID No: **P150361**
Assignment Title: **Provision of Consultancy Updating of Environmental and Social Impact Assessment for the Implementation of Water Supply and Sanitation Improvement Projects for Tanga City**

Tender No.**ME-011/2020-2021/C/20**

Reference No. **TZ-MOW-195725-CS-CQS**

1. This request for expression of interest follows the General Procurement Notice for the project that appeared in the United Nations Development Business; Issue No. WB5803 – 12/16 of December 21, 2016.

2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank towards the cost of the Water Sector Support Project (WSSP II) which is part of the Second Water Sector Development Program (WSDP II), and intends to apply part of the proceeds for consulting services.

3. The consulting services ("the services") include Provision of Consultancy Updating of Environmental and Social Impact Assessment for the Implementation of Water Supply and Sanitation Improvement Projects for Tanga City. The assignment is also expected to result into the development of the Environmental and Social Management Plan (ESMP) as well as Health and Safety Management Plan (HSMP) for the implementation of the entailed project activities. The assignment will be undertaken in a period of Ten (10) calendar weeks.

4. The Ministry of Water (MoW) now invites eligible consultants to express their interest in providing the services. Interested Consultants should provide information indicating that they are qualified to perform the services. The short listing criteria are:(i) core business of the firm and the number of years in business;(ii) experience in similar assignment (Environmental and Social Impact Assessment (ESIA)) (iii) experience of having worked in sub-Saharan Africa or similar environment; (iv) technical and managerial capability of the firm (Provide only the structure of the organization, general qualifications and number of key staff. Do not provide CV's of staff since key experts will not be evaluated at the short-listing stage). Consultants may associate with other firms in the form of a joint venture or a sub consultancy to enhance their qualifications.

5. The attention of interested Consultants is drawn to paragraph 1.9 of the World Bank's Guidelines: Selection and Employment of Consultants [under IBRD Loans and IDA Credits & Grants] by World Bank Borrowers, January 2011, revised July 2014 ("Consultant Guidelines"), setting forth the World Bank's policy on conflict of interest.

6. A Consulting Firm will be selected in accordance with the Consultant Qualification Selection (CQS) Method set out in the World Bank Guidelines.

7. Interested consultants may obtain further information at the address below during office hours from 8:00 to 15:30 hours, Monday to Fridays inclusive, except on public holidays.

8. Expression of Interest marked **"EXPRESSION OF INTEREST FOR PROVISION OF CONSULTANCY UPDATING OF ENVIRONMENTAL AND SOCIAL IMPACT ASSESSMENT FOR THE IMPLEMENTATION OF WATER SUPPLY AND SANITATION IMPROVEMENT PROJECTS FOR TANGA CITY"** should be delivered in a written form to the address below (in person, or by courier, or by e-mail) by 27th January 2021 at 14:00 hour's local time.

Physical Address:
The Secretary Ministerial Tender Board
Ministry of Water,
Kolon Building adjacent to DUWASA Head Office, PMU Offices,
Chimwaga Road,
40473 Dodoma, Tanzania

Attention:
Dr. Christopher P. Nditi
Director of Procurement Management Unit
Telephone: **+255 716 308473**
E-mail: pmu@maji.go.tz

**PERMANENT SECRETARY**
**MINISTRY OF WATER**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchangiaji ujenzi madarasa ni jukumu la wote

**DESEMBA** 18, mwaka jana serikali ilitoa agizo kwa halmashauri zote nchini kuhakikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa unakuwa endelevu kwa sababu idadi ya wanafunzi walioandikishwa na wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza inafahamika.

Iliagiza ifikapo Februari 28, mwaka huu ujenzi wa vyumba vya madarasa uwe umekamilika na kuwezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaingia darasani.

Kila halmashauri imetakiwa kujenga vyumba vya kutosha vya madarasa kuondoa adha ya wanafunzi kukosa nafasi ya kuanza masomo kutokana na ukosefu wa vyumba hivyo.

Akitoa agizo hilo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitaka kila mtoto wa Kitanzania aliyefaulu aende sekondari na jukumu la halmashauri ni kuhakikisha inajenga vyumba vya kutosha vya madarasa na walimu waendelee kufanyakazi kwa bidii kwa kuwa serikali inatambua na kuthamini kazi nzuri wanayoifanya ambayo inawezesha kuongeza idadi ya wanafunzi wanaofaulu kila mwaka.

Katika kutekeleza agizo hilo wadau mbalimbali wa elimu wamejitokeza kuisaidia serikali kukamilisha lengo hilo ili kila mtoto aliyefaulu kujiunga na sekondari asikose nafasi hiyo.

Mashirika, kampuni, watu binafsi, taasisi, viongozi mbalimbali wa kisiasa na kiserikali ni baadhi tu ya wadau wa elimu walioamua kujitoa kuisaidia serikali kutimiza lengo hilo la kila mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na sekondari asikose nafasi hiyo.

Misaada hiyo ni pamoja na vifaa vya ujenzi, fedha taslimu na nguvu kazi.

Moyo huu wa kujitoa wa mashirika na taasisi mbalimbali uwe chachu ya kila mwananchi kujitoa kuchangia ujenzi huo wa vyumba vya madarasa.

Juhudi hizo zisipofanikiwa watoto watakaokosa nafasi ya kuingia darasani kwa kukosa vyumba, wataachwa katika mazingira hatarishi.

Ndoto yao ya malengo waliyojiwekea itakuwa imezima na kuwaathiri kisaikolojia na wengine kujiingiza katika mambo yasiyofaa.

Wapo wananchi wanaojitoa kuchangia ili kutimiza malengo ya watoto wao, lakini kuna baadhi wanakwamisha kwa kutumia michango hiyo kuitafuna kwa manufaa yao.

Katika tukio moja lililoripotiwa juzi, kuna baadhi ya kamati zilizoundwa kusimamia makusanyo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na kuamua kutafuna fedha hizo, hali inayorudisha nyuma ari ya wananchi hao kuchangia.


Ikumbukwe kuwa ujenzi huo utanufaisha pia vizazi vijavyo ambao utanusuru wimbi la watoto wanaobaki mtaani na kujiingiza katika makundi ya kihalifu.

Tukumbuke miaka ya nyuma wakati watoto walipokuwa wakimaliza elimu ya msingi ilikuwa ni kipindi cha mawakala cha kuwatafuta na kuwapeleka kutumikishwa kazi za ndani.

Serikali kwa sasa imeondoa tatizo hilo kwa kuhakikisha kila mtoto anapata elimu ya bure na hiyo imesababisha watoto wengi kuchaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari hali inayofanya kuwapo na upungufu wa vyumba vya madarasa kwa sababu ya idadi kubwa ya watoto wanaochaguliwa.

Ushirikiano unaoonyeshwa na wadau mbalimbali uungwe mkono kutimiliza lengo la kila mtoto aliyechaguliwa kuingia sekondari anapata nafasi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vijana wekezeni kwenye kilimo, kwa kweli nacho kinalipa sana

Na Maulid Mmbaga

**KILIMO** kina maana pana inayojumuisha mifumo ya uzalishaji mimea, ufugaji wa wanyama na uvuvi wa samaki.

Hata hivyo kwa kuwa maji hayapatikani kila mahali, kilimo cha mimea ndicho kinachoenda sambamba na ufugaji wanyama.

Watu hupanda mimea na kuitunza hadi mavuno hasa kwa uzalishaji chakula cha binadamu na lishe ya wanyama, pia kwa shabaha ya kupata malighafi mbalimbali zinazotumiwa kwa kutengeneza nguo za watu.

Kutokana na changamoto ya ajira inayowakabili baadhi ya Watanzania hususani vijana kulikabili tatizo hilo, ni vyema kujiwekea utaratibu wa kuwekeza katika kilimo cha biashara na kujiingizia kipato, kwani ni mojawapo ya sekta zinazo tegemewa nchini.

Ni sehemu ya shughuli za mwanadamu, inayogawanyika katika makundi makuu mawili, ambayo ni kilimo cha chakula na biashara.

Hivyo, kilimo kinamsaidia mkulima kupata mazao kwa ajili ya chakula na mengine kwa ya biashara, ambayo yanaweza kumwingizia kipato na anajikwamua kimaisha. Kipato hicho, ndicho husaidia kukuza uchumi wa nchi.

Sekta hiyo ndiyo inainua uchumi mkubwa kwa mataifa mengi, hasa yaliyoko katika daraja la chini. Ni mara zote serikali hushirikiana na wadau mbalimbali wanaojihusisha nayo, katika kuipa vipaumbele zaidi. Mwisho wa siku ni kumpisha adui njaa.

Serikali pamoja na wadau, wanazidi kuongeza zana za kilimo ili watu wapate mazao ya biashara na chakula na kuwafanya wote wanaojihusisha na mchakato huo wanufaika kiuchumi.

Pia serikali daima imekuwa katika harakati za kutoa elimu inayohusu kilimo bora, kama kitega uchumi kinachowasaidia kupatia mazao na kipato cha kuendesha maisha yao binafsi ya kila siku.

Rai ninayowapa wananchi ni kwamba, wakulima wapewe kipaumbele katika suala la mikopo ya pesa, pindi wanapokuwa na uhitaji ili waweze kujikwamua kwa kununua pembejeo na vifaa mbalimbali vinavyowasaidia katika kilimo.

Lingine mbele ya nafsi yao, ni kwamba wanatakiwa kujikita katika kilimo cha umwagiliaji si tu kutegemea mvua pekee.

Bunge la Tanzania lilishaidhinisha Sh. bilioni 229.8 kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka wa fedha uliopo, inayokusudia kutekeleza vipaumbele 10, vikiwamo kuzalisha mbegu bora kwa ajili ya wakulima nchini.

Bajeti hiyo iliyokwishaanza kutekelezwa Julai Mosi na mpango wake ukiwa na msisitizo kwenye kilimo kitakachohakikisha usalama wa chakula, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula na upatikanaji malighafi ya viwanda.

Vipaumbele hivyo vinatajwa kuwa ni kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), inayolenga kuimarisha vyuo, vituo vya mafunzo na utafiti wa kilimo.

Mengine ni kudhibiti visumbufu vya mimea, huduma za ugani, usajili wa wakulima na bima ya mazao, kuboresha mifumo ya kitaasisi, bodi na sheria za kilimo kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo na kuunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kuendeleza kilimo cha kibiashara.

Kwa mujibu wa mkakati huo wa kibajeti, inaonyesha dhahiri umuhimu wa sekta ya kilimo kitaifa, hivyo vijana pamoja na Watanzania kwa ujumla, wanaopaswa kuwekeza zaidi katika hilo.

Sekta hiyo ikiwa ni moja ya harakati za kujikwamua kiuchumi na kuuepuka umaskini, kadhalika itasaidia kupunguza kama sio kumaliza kabisa tatizo la ajira nchini.

Pia serikali iwatazame wakulima katika suala la masoko ya mazao wanayoyazalisha waweze kuyauza kwa bei inayoendana na mazao yao, ili kuepuka walanguzi wanaochangia kuwadidimiza kiuchumi na kurudisha nyuma maendeleo ya taifa.

# HABARI PICHANI



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge  (kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa IPP, Joyce Luhanga  baada ya kutembelea ofisi za magazeti ya kampuni ya The Guardian Ltd jijini Dar es Salaam jana.



Mkurugenzi wa EATV/ na Radio, Regina Mengi, akimkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge.



Naibu Mkurugenzi wa Radio One/ Capital Radio, Abdallah Mwaipaya, akifafanua jinsi wanavyorusha matangazo yake.



Mkurugenzi wa Radio One/Capital Radio, Deo Rweyunga, akimweleza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam jinsi redio hizo zinavyofanya kazi.



Mkuu wa Mkoa wa Dares Salaam, Abubakar Kunenge, akimsikiliza Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul.



Mussa Fumbuka Mtaalam wa Mifumo wa Kituo cha ITV, akimweleza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam jinsi habari inavyorushwa. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**

ARUSHA TECHNICAL COLLEGE

*(Registered by the Vocational Education and Training Authority)*

KIKULETWA RENEWABLE ENERGY RESEARCH AND TRAINING CENTRE

**INVITATION FOR ADMISSION INTO ARTISANS PROGRAMMES FOR THE ACADEMIC YEAR 2021.**
**KIKULETWA CAMPUS**

Kikuletwa Renewable Energy Training and Research Centre is part of Arusha Technical College established for the purpose of Training and Research in Renewable Energy Skills including Hydropower Turbine Testing and Calibration.
The center is now inviting applications for academic year 2021 from qualified candidates for Artisans programme leading to National Vocation Awards Levels I-III. The Training will be conducted at Kikuletwa Campus in Hai District.

**1. PROGRAMMES**
a) Hydropower Plants Operation and Maintenances NVA I-III
b) Renewable Energy NVA I
c) Domestic Electrical Installation NVA I-III
d) Plumbing and Pipe Fitting (Ufundi Bomba) NVA I-III and
e) Masonry and Brick and Laying NVA I-III
f) Solar PV Systems Installation NVA I-III
g) Bio-energy systems construction NVA I-III
h) Wind power plant installation NVA I-III

**2. ENTRY REQUIREMENTS**
Admission to this programme is open to candidates who have Primary School Standard VII Certificate or; Ordinary Secondary School Education or; Apprentices from the industry with field experience in hydropower generation, maintenance, operation or manufacture of hydropower turbines for at least one year.

**3. MODE OF APPLICATION**
Application forms can be obtained from the Office of Registrar at the Arusha Technical College or can be downloaded from the College **website: http://www.atc.ac.tz.** Application forms will only be considered if accompanied by:
(i) A non-refundable application fee of TZS. 20,000/= (TZS Twenty thousand only)
Which is paid by using CONTROL NUMBER which is available in our College website (www.atc.ac.tz)
You will be required to visit our mentioned website and then click link written ICT SERVICES in bar line, the after you will click electronic payment and fill well a form that will appear and request your CONTROL NUMBER
After a short time, the applicant shall receive a "CONTROL NUMBER" which will be used to deposit the application fee to any NMB or CRDB branch or agent all over the country.
NB; In writing an amount to pay you are not allowed to add any punctuation mark ie (' , / =) in the figure you have written. Let only the numbers appear ex. 20000

**OTHER REQUIRMENTS**
(ii) Certified copies of relevant certificates such CSEE, Academic Transcripts/National Examination statements of results or results slip.
(iii) Birth Certificate
(iv) School Leaving Certificate
(v) Two coloured personal passport size photographs taken within the last six months.

**4. FEES FOR PRIVATE SPONSORSHIP**
The fee structure is as follows:

a) Fee for day students is as shown in the table below follows:

| S/N | MAELEZO | NVA I | NVA II | NVA III |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuition Fee | 400,000 | 400,000 | 400,000 |
| 2 | Registration | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 3 | Identity Card | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 4 | NHIF-(Bima ya Afya)* | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| 5 | Student Organization fee | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 6 | Caution Money | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| **7** | **VETA Examination fee** | 12,000 | 17,000 | 22,000 |
| | **Total with NHIF** | **502,400** | **507,400** | **512,400** |
| | **Total without NHIF** | **452,000** | **457,000** | **462,000** |

***NHIF for students who are not covered yet***

b) Fee structure for boarding students is as shown in the table below:

| S/N | MAELEZO | NVA I | NVA II | NVA III |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fee | 400,000 | 400,000 | 400,000 |
| 2 | Registration | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 3 | NHIF-(Bima ya Afya)* | 50,400 | 50,400 | 50,400 |
| 4 | Identity Card | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 6 | Student Organization fee | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 7 | Caution Money | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| 9 | Accommodation | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| | **VETA Examination fee** | 12,000 | 17,000 | 22,000 |
| | **Total with NHIF** | **552,400** | **557,400** | **562,400** |
| | **Total without NHIF** | **502,000** | **507,000** | **512,000** |

***NHIF for students who are not covered yet***
***There are limited accommodation facilities for female students only***
***The Canteen will offer Meals services to all students at their own costs***

**5. CLOSING DATE**
Closing date for receiving application forms is **31th January, 2020. No consideration will be made to late applicants.**

**6. SUBMISSION OF APPLICATIONS**
All applications should be addressed to:
The Registrar
Arusha technical College
P. .O.Box 296,
Arusha-Tanzania

**7. WARNING**
Submission of forged certificates or any false information is criminal offence and will be dealt with according to the law.

**8. ENQUIRIES**
All enquiries about admission should be addressed to:
Admission Officer, Arusha Technical College, P.O. Box 296, Arusha, **Tel.** +255 27 2503040
**Fax:** +255 27 2548337
**E-mail:** admissions@atc.ac.tz mobile 0715141650, or 0762405112 or 0689639452 from 8:00 AM to 5:00 PM only

# RC ashangaa bili ya maji Polisi, Magereza 3,000/- kila mwezi

**Na Thobias Mwanakatwe**

SERIKALI ya Mkoa wa Songwe, imeshangazwa na hatua ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Miji ya Vwawa na Mlowo kuzitoza taasisi za Polisi na Magereza bili za maji Sh. 3,000 kwa kila mwezi huku mwananchi wa kawaida akipewa bili ya Sh. 20,000.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Nicodemas Mwangela, alibainisha hayo juzi mbele ya Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyezuru kukagua miradi ya maji katika mkoa huo.

"Siyo jambo la kawaida. Kwa mfano, kambi ya polisi inayohudumia zaidi ya watu 60 hadi 70 halafu kwa mwezi ndiyo wanapelekewa bili ya elfu tatu (Sh. 3,000), lakini mwananchi mmoja anapewa bili ya elfu ishirini (Sh. 20,000)," alisema.

Brigedia Mwangela alisema katika suala hilo, tatizo siyo polisi bali ni ubovu wa menejimenti ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vwawa na Mlowo na kwamba kutokana na hali hiyo, anaiomba Wizara ya Maji kufanya mabadiliko ya viongozi katika mamlaka hiyo.

Alisema kila taasisi inatakiwa ichangie kulingana na inavyotumia maji ili fedha zinazopatikana zitumike kupanua huduma ya maji kwa wananchi.

Alisema Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Songwe (RUWASA) inafanya kazi vizuri katika utoaji wa huduma kwa wananchi, ambapo hadi sasa inatoa huduma hiyo kwa asilimia 75.5 wakati Mamlaka ya Maji Safi Vwawa na Mlowo inatoa huduma kwa asilimia 44.5. "Kwa mkoa mzima upatikanaji wa maji ni asilimia 70 ambapo asilimia hizo zimeshushwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika miji ya Vwawa na Mlowo licha ya kwamba walipata Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa wananchi," alisema.

Aliongeza kuwa hata ukusanyaji wa mapato, mamlaka hiyo haiko vizuri kulinganisha na idadi ya watu wanaotumia maji katika miji hiyo na yote hiyo ni kutokana na udhaifu kwenye menejimenti.

Kufuatia hali hiyo, Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca, alichukua hatua kumsimamisha kazi Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingita Wilaya ya Mbozi, Akiba Kibona.

# Waziri ataka vyuo vijibu mahitaji ya nchi

**Na Gwamaka Alipipi**



WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (pichani), amevitaka vyuo vya teknolojia nchini, kutoa kozi zinazokwenda kutibu, kujibu hitaji la soko la nchi, sambamba na kuangalia mahitaji yenye maslahi.

Amesema kwa sasa Tanzania imeingia katika uchumi wa kati, hivyo haiwezi kuendelea kuwa tegemezi kwa nchi zingine katika masuala ya teknolojia.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mahafali ya 14 ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), 1,096 wakihitimu katika fani mbalimbali.

Dk. Ngugulile alisema: "Nchi inapokuwa katika uchumi wa kati, tunahitaji wataalamu wa ufundi na teknolojia, tunataka tuwe sehemu ya dunia, tuangalie katika biashara ya mtandao, tutoe kozi zinazokwenda kutibu, kujibu soko letu za Tanzania.

"Tunataka kuona vyuo vyetu vikija na ubunifu utakaoweza kuleta matokeo mazuri ya kiuchumi hususani wakati huu ambao viwanda vingi bado vinaendelea kuanzishwa."

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa James Mdoe, alisema ili kuzalisha wataalamu mbalimbali, DIT imejikita katika masuala ya ubunifu kwa kubuni utafiti.

Alisema pamoja na uwapo wa ubunifu huo, bado kuna matatizo mbalimbali yanayowakabili kama taasisi ili kufanikisha ubunifu wenye ubora unaoleta chachu kwa taifa.

Alisema katika kuhamasisha ubunifu na utafiti, wizara imekuwa ikitoa ushirikiano wa karibu kwa taasisi na vyuo vilivyopo nchini, ikiwa ni pamoja na kuwapeleka wabunifu katika taasisi mbalimbali zenye viwango vya juu vya ubunifu.

Kiongozi huyo alibainisha kuwa hadi sasa, wabunifu 130 wameshapelekwa katika taasisi hizo kwa ajili ya kupata ujuzi, lengo kuu likiwa kuwa na wabunifu wengi watakaoliletea taifa manufaa.

Mkuu wa DIT, Profesa Praksedis Ndomba, alisema katika kuwajengea uwezo wa kimafunzo na kitaaluma wanafunzi wake, DIT imeingia mkataba wa ushirikiano na taasisi zaidi ya 30 kutoka ndani na nje nchi, unaowawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo.

Alisema katika kuhakikisha taasisi hiyo inafikia malengo yake, wamekuwa karibu na taasisi hizo ambazo baadhi zipo juu kitaaluma, lengo likiwa kuwajengea uwezo wanafunzi pamoja na taasisi kwa ujumla.

Alisema ili kuzidi kufikia malengo yake ya utoaji wa elimu, DIT imejiimarisha katika nyanja mbalimbali ikiwamo ujenzi na ukarabati wa majengo na maabara kwa ajili ya ufundishaji.

Profesa Ndomba alisema tayari serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 37 maalum kwa ajili ya kufanikisha masuala yote muhimu chuoni hapo ikiwamo ujenzi wa majengo ili kuiwezesha taasisi hiyo kufikia malengo yake.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

ISO 9001: 2015 IMETHIBITISHWA

# TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI KUHUSU MADAI KUWA TRA IMEPANDISHA KODI ZA MAGARI YALIYOTUMIKA (USED MOTOR VEHICLES) YANAYOINGIA NCHINI

Kumekuwa na taarifa zikisambaa kwenye mitandao ya kijamii, zikiambatana na madai kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") imeongeza ushuru kwa magari yanayoingia hapa nchini, yakitajwa baadhi ya magari kuongezwa kodi ambapo ni uelewa wetu kuwa mtoa taarifa alikuwa akiongelea magari yaliyotumika (used motor vehicles).

Tunapenda kutaarifu umma kuwa ukadiriaji wa kodi kwa bidhaa zinazoingia nchini, yakiwemo magari, hufanywa kwa kuthaminisha bidhaa hizo na hatimaye kukokotoa kodi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria za kodi kama zilivyo tungwa na kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uthaminishaji wa bidhaa hufanyika kwa mujibu wa **Kifungu cha 22 cha Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 (iliyorejewa Mwaka 2019),** kikisomwa pamoja na Jedwali la Nne la Sheria hiyo, ambalo limeainisha Kanuni za uthaminishaji ambazo ndizo hutumika kwenye kuthaminisha bidhaa zinapoingia hapa nchini. Kimsingi thamani (au bei) ya bidhaa inayopaswa kutumika kukokotoa kodi kwa mujibu wa Sheria za Forodha ni bei ambayo muingizaji **amelipa au anapaswa kuilipa kwa bidhaa** hiyo kwa wakati huo. Ili bei hiyo ikubalike na kutumika kiforodha kwa bidhaa hiyo, muingizaji wa bidhaa, ni sharti atoe Ushahidi Madhubuti utakaothibitisha pasipo shaka kuwa amelipa au anapaswa kulipa bei hiyo na ikiwa hana ushahidi kanuni za ukadiriaji zinaelekeza kutumiwa kwa bei za bidhaa kama hizo au zinazofanana na hizo zilizoingia au zinazoingia nchini kutoka kwa muuzaji aliyemuuzia au kwa muuzaji mwingine nchi alikonunua katika kipindi husika kawaida ndani ya muda wa miezi mitatu (3).

Pia, uthaminishaji wa magari yaliyotumika hufuata msingi wa Sheria wa uthaminishaji ambapo bei zake na viwango vinavyotozwa kwenye kila gari huwekwa kwenye tovuti ya TRA ili kuwasaidia waingizaji kukokotoa kodi inayoweza kulipwa kwenye gari husika wakati ambapo gari litakapokuwa linaingia ndani ya nchi. Aidha, ni vyema ikaeleweka kuwa endapo kutakuwa na Ushahidi madhubuti wa bei halisi, Mamlaka, kwa mujibu wa Sheria bado ina wajibika kutoza ushuru gari hilo kwa bei halisi iliyolipwa au inayosapaswa kulipwa kwenye gari hilo. Sheria ya uthaminishaji inaitaka TRA kurejea bei hizo kila baada ya kipindi fulani ili kuhuisha kanzi data za bei za bidhaa hizo na uamuzi wa kuongezwa au kupunguza hufikiwa kwa kuangalia bei halisi ya bidhaa husika kwa kipindi hicho kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, zikiwemo tovuti za makampuni yanayouza magari hayo.

Katika kutekeleza jukumu la kupitia upya bei za magari yaliyotumika, ili kwenda na bei halisi za magari hayo, **kuanzia Januari 2021** yapo magari machache ambayo bei zake zimeongezeka kutokana uthaminishaji uliozingatia bei halisi za magari hayo hali ambayo imesababisha kuongezeka kwa ushuru na magari mengi bei zimepungua. Kimsingi ongezeko hilo limetokana na bei halisi ya magari husika na hivyo haimaanishi kuwa TRA imeongeza ushuru wa magari.

Sambamba na hilo tunautaarifu umma kuwa magari yaliyotumika pia hutozwa **ushuru wa bidhaa kutokana na umri wa gari (excise duty on age)** ambapo umri wa magari huhesabiwa kwa kufuata mwaka wa kalenda, kwa upande wa magari madogo **(private cars), magari yenye umri wa miaka 8-9, pamoja na kodi zingine, hutozwa ushuru huo wa bidhaa kwa asilimia 15% na gari yenye umri zaidi ya huo hutozwa kwa asilimia 30%.** Hivyo, ikiwa muingizaji aliagiza gari binafsi lenye umri wa miaka 9 mwaka 2020 na likaingia nchini mwaka 2021 litatozwa ushuru wa bidhaa kwenye umri wa asilimia 30% badala ya asilimia 15% ambayo ingetozwa ikiwa gari yake ingewasili kabla ya mwaka 2021. Kwa sababu hiyo, waingizaji wa magari yenye umri huo walioagiza mwaka 2020 na gari kuingia mwaka 2021 ni wazi kuwa kodi kwenye gari aliloagiza itaongezeka. **Hivyo, tunautaarifu umma kuwa hakuna kiwango cha kodi kilichoongezwa kwenye magari.**

Aidha, ili kuhakikisha TRA inatenda haki kwenye kutekeleza majukumu ya uthaminishaji wa bidhaa mbalimbali zinazoingia na maswala mengine ya kiforodha wakati wa ugomboaji wa bidhaa zilizowasili bandarini, kwenye viwanja vya ndege na mipakani, ndani ya Mfumo Unganishi wa Forodha Tanzania (TANCIS) muingizaji kupitia wakala wake wa forodha (CFA) ana haki ya kupinga bei endapo ataona hakutendewa haki na maofisa wetu watapitia pingamizi lake kupitia taarifa na nyaraka mbalimbali zilizowasilishwa kwenye TANCIS na kutolea uamuzi. Ikiwa ataona bado hajaridhika na uamuzi uliotolewa, ama muingizaji mwenyewe au kupitia kwa wakala wake wa forodha, anayo haki ya kuwasilisha kwa maandishi rufaa au malalamiko yake kwa Kamishna wa Forodha.

Pamoja na ufafanuzi wa hapo juu, tunapenda kuutahadharisha umma kuwa, TRA katika kutekeleza jukumu lake la uthaminishaji wa bidhaa mbalimbali, na hasa magari, imebaini udanganyifu kwa baadhi ya waingizaji wasio waaminifu kuwasilisha **Ankara (Invoice)** za kughushi ili kulipa kodi kidogo wakati wakijua bei waliyonunulia ni kubwa kuliko waliyotamka kwenye kadhia ya forodha ya gari husika. Ili kufanikisha udanganyifu huo, baadhi ya waingizaji, wakati wakituma pesa za kununulia magari hayo nje ya nchi huzigawanya zaidi ya mara moja na kwa lengo la kuwasilisha TRA ushahidi wa kutuma pesa kupitia benki Telegraphic Transfer (TT) ya muamala mmoja unaoendana na bei iliyomo kwenye Ankara aliyoghushiwa. Tunapenda kuwataarifu kuwa kufanya hivyo ni kosa chini ya **Kifungu cha 203 cha Sheria ya Forodha** kikisomwa pamoja na **Kifungu cha 84 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**. Aidha, udanganyifu huo unadhohofisha juhudi za TRA za kukusanya mapato ya Seikali na hatimaye kudhohofisha nguvu za Serikali za kutekeleza miradi ya maendeleo na kuhudumia wananchi wake. Hivyo, TRA itachukua hatua stahiki kwa wadanganyifu hao kwa mujibu wa Sheria tajwa

Tunaendelea kuthamini mchango wa waingizaji wa bidhaa nchini na walipakodi wengine wote kwenye ujenzi wa uchumi wa nchi yetu. Hivyo, tunawataarifu kuwa wakati wote TRA tutaendelea kuwahudumia kwa kutumia utaratibu uliowekwa kwa mujiu wa Sheria. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma zetu, walipakodi wanaweza kutufikia kwa kupiga simu bure kupitia namba **0800-750-075 au 0800-780-078, barua pepe** huduma@tra.go.tz au kutuma ujumbe kupita namba ya **WhatsApp +255-744-233-333.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Imetolewa na:**

**IDARA YA ELIMU NA HUDUMA KWA MLIPAKODI**

# DC awataka watendaji kuunda vikundi vya usafi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, amewataka watendaji wa kata kusimamia uundaji wa vikundi vya usafi kwenye maeneo yao.

Akiongea na Nipashe jana mjini hapo, Ntemo alisema vikundi hivyo vinavyosaidia kuimarisha usafi kwenye maeneo yao na kuepukana magonjwa ya mlipuko.

Alisema kila mtendaji anatakiwa kuhakikisha vikundi hivyo vya uzoaji taka vipo kwenye maeneo yao na vinafanya kazi.

Alisema viongozi wa shule pia wanatakiwa kuzingatia usafi wa mazingira hususani kipindi cha mvua na msimu wa maembe unaoendelea.

Mkurugenzi wa Mji wa Kibaha, Jenifa Omolo, akizungumzia kaya ambazo hazina vyoo, alisema ipo kampeni inaendelea kuhakikisha kila nyumba ina choo.

Omolo alisema wapo maofisa afya wanaoendelea na kampeni ya kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora lengo ni kuwaepusha wananchi na magonjwa ya mlipuko.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa Mtaa wa Tangini, Shauri Yombayomba, alisema zipo baadhi ya kaya katika mtaa wake hazina vyoo huku kaya nyingine zikikabiliwa na uhaba wa vyoo kutokana na idadi kubwa ya watu.



Wateja wakichagua matikiti katika Soko la Vetenari jijini Dar es Salaam jana, tikiti moja linauzwa kwa Sh. 3,000 hadi 2,500.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bil. 1.6/- kuinufaisha Mara maji

**Na Timothy Itembe,** MARA

WANANCHI wa wilaya za Mkoa wa Mara wanatarajiwa kunufaika na Sh. bilioni 1.6 zilizotolewa na Wizara ya Maji kutekeleza miradi ya maji.

Waziri wa Maji, Juma Aweso, alisema hayo mbele ya wananchi waliohudhuria ziara yake ya kukagua miradi mkoani hapo.

Alisema serikali imejipanga kutekeleza sera ya maji kumtua mama ndoo kichwani na kila wilaya ndani ya mkoa wa Mara imetengewa Sh. bilioni 1.6.

Aweso alisema hayo baada ya kusomewa taarifa za utekelezaji wa miradi ya maji kusuasua katika mkoa Mara na kuwataka wahandisi aliowaita kuwa wazembe kuachia ngazi kabla rungu la utumbuaji halijawafikia.

Waziri huyo alitumia nafasi hiyo kuwaahidi wananchi wa wilaya Rorya kuwaletea gari kwa ajili ya kushughulikia matatizo yanayowakumba ya upatikanaji wa maji.

"Wizara ya Maji imetoa gari ili kusaidia huduma za maji Wilaya ya Rorya, Mkoa wa Mara na watalipata ndani siku tatu kuanzia leo (jana) hiyo ni kutokana na changamoto kubwa niliyosomewa ambayo inasababisha miradi ya maji kuchelewa kukamilika kwa wakati kutokana na umbali mrefu uliopo kuifikia," alisema Aweso.

"Hatuwezi kushindwa kutekeleza huduma za wananchi kwa sababu ya ukosefu wa gari, wizara italeta gari kwa ajili ya kusaidia ufuatiliaji wa miradi hii na hata hivyo, kuna gari zinakuja lazima moja liletwe huku," alisema waziri Aweso.

Pia Waziri Aweso alitembelea miradi ya maji vijiji vya Komuge, Kiamwami, Kirogo na Shirati wilayani hapo.

Mhandisi Evaristo Mgaya, akitoa taarifa ya mradi wa maji wa Komuge, alisema ulianza mwaka 1975 kwa ajili ya vijiji vya Kyamwame, Komuge, Kuruya, Irienyi na Baraki, lakini ulikwama kutoa huduma ya maji mwaka 2009 kutokana na uchakavu wa bomba kuu.

Mgaya alitaja moja ya matatizo yanayowakwamisha kuwa ni uhaba wa magari kwa ajili ya usafiri wa uhakika kwa ufuatiliaji na usimamizi, mazingira ya kufanyia kazi kutofika kirahisi na kuchelewa kurudishwa kwa huduma ya umeme.

Mbunge wa Jimbo la Rorya, Jafari Chege, alimwomba Waziri wa Maji kuwarudisha makandarasi waliokuwa na tenda awali na kulipwa zaidi ya asilimia 80 ya fedha anazodai wamalizie miradi sehemu iliyobaki badala ya kumleta mkandarasi mpya ambaye atalazimika kugharimu pesa nyingine.

Chege alisema ucheweshwaji wa vifaa hususani mabomba ya usambazaji wa maji unakwamisha miradi kukamilika kwa wakati.

# Madiwani wabadili matumizi fedha kujenga madarasa

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MADIWANI wanaounda Halmashauri ya Wilaya mkoani Pwani, wamefanya kikao maalumu cha kubadilisha matumizi ya fedha ili kujenga vyumba vya madarasa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi 3,637 waliokosa nafasi kutokana na uhaba wa madarasa hayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani.

"Wanafunzi mwaka huu 7,327, wamechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, lakini changamoto ya vyumba vya madarasa inasababisha watoto 3,700 kujiunga na masomo," alisema.

Aliongeza kuwa, baada ya kuona watoto 3,627, wamekosa nafasi baraza likakutana na kufanya uamuzi ili watoto waende shule.

Katika baraza hilo, madiwani wote wameridhia matumizi ya fedha yabadilishwe ili kujengwa kwa vyumba vya madarasa ambavyo vitawasaidia wanafunzi hao.

Mkuu wa wilaya hiyo, Filbeto Sanga, alisema vyumba vya madarasa vitajengwa kwenye shule hizo za sekondari kwa kuongezea idadi.

Alisema agizo la serikali linataka Februari 28, watoto wawe kwenye vyumba vya madarasa na vilivyo na viti.

"Maeneo mengi yanachangamoto, serikali imetoa maagizo watoto waliofaulu mwaka huu wawe darasani," alisema.

Aliongeza kuwa mwakani idadi ya watoto itaongezeka na kuwa 14,000 na kwamba watahakikisha wanaochaguliwa wanaingia shule kama kawaida.

Sanga aliwaonya walimu kuwatoza michango yoyote wanafunzi wanaokwenda kuanza shule.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mohamed Mwela, alisema tatizo la elimu Mkuranga ni kubwa kutokana na watoto wengi kutoka jijini Dar es Salaam kwenda wilayani humo kusoma. Pia, aliwapongeza madiwani kwa kukubali kujengwa vyumba vya madarasa katika shule ambazo zina nafasi ya kuongeza madarasa hayo.



Ukurasa 12

Mihogo ya kukaanga na samaki ilivyoshika kasi mitaani jijini Dar, ukiibua uchumi mpya



Ukurasa 14

**Chimbuko 1947; misitu, mapango ya vita kuu, inaongoza Afrika kwa vipepeo**

BUFE
IJUMAA JANUARI 8, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Kim Jong-un: Korea Kaskazini tumefeli kila sekta ya kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu**

KIONGOZI wa Korea Kaskazini Kim Jong-un amekubali kuwa mpango wake wa kiuchumi wa miaka mitano kwa nchi hiyo umeanguka, pasipo mafanikio.

Alikuwa akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha dharura cha chama chake cha Workers' Party, ambacho ni cha nane katika historia ya nchi hiyo, anasema nchi ilijitenga na kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa, akitamka kila sekta imeanguka.

Korea Kaskazini ilifunga mipaka yake Januari mwaka jana, kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona, licha ya madai kwamba hakujawahi kuwa na maambukizi ya virusi hivyo nchini humo.

Hatua hiyo, inaelezwa imesababisha kujitenga na majirani zake ambayo pia ni washirika wake wa karibu, China na kufanya biashara kati ya nchi hizo mbili kudorora kwa asilimia 80.

Aidha, kimbunga na mafuriko zilizolikumba taifa hilo, zimesababisha nyumba na mazao kuharibika ndani ya huko Korea Kaskazini na bado imewekewa vikwazo vikali vya kimataifa, ikiwamo mpango wake wa nyuklia, unaonyooshewa vidole na wapinzani hasa wa Magharibi.

Sio jambo la kawaida kwa Kim kukubali makosa yake - hatua ambayo imekuwa kama utambulisho wake amesema Laura Bicker.

Taarifa kupitia televisheni zinaonyesha wakiwa kwenye mkutano katika mji mkuu wa Pyongyang uliokuwa umejaa maelfu ya wanachama na hakuna aliyekuwa amevaa barakoa walipokuwa wamesimama kupiga makofi wakimkaribisha Kim alipoingia mkutanoni.

Katika hotuba yake, Kim alisema mkakati wake wa miaka mitano alioutangaza mwaka 2016, umekosa kufanikiwa kwa karibu kila sekta na ni lazima mtu akubali kuwa alikosa.

Alitoa wito wa kujitegemea na kusifu wanachama kwa kukabiliana na tishio la janga la virusi vya corona.

Korea Kaskazini iliiambia Shirika la Afya Duniani (WHO), kuwa maelfu ya watu wanashukiwa kupata maambukizi, lakini haijawahi kukubali kuwa imethibitisha chochote cha maambukizi ya virusi vya corona.

Hata hivyo, bado haijafahamika itakabiliana vipi na changamoto kwa nchi hiyo katika kipindi cha miongo kadhaa cha misukosuko hasa ya corona.

Kim alitarajiwa kutangaza mpango mpya wa miaka mitano katika mkutano huo na inawadia wiki mbili tu kabla ya Rais mteule wa Marekani, Joe Biden, kuchukua madaraka na nduguye, Donald Trump kufungasha virago.

Inadaiwa, walau Rais Reumop kuna sentensi wakielewana, ingawa majadiliano yao kuhusu mpango wa nyuklia wa Korea Kaskazini haukufika mbali 'kihivyo.'



Wajumbe wa kikao cha kisiasa, ambacho kiongozi huyo alikiri. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Kiongozi Mkuu wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un.

BIASHARA

# Mihogo ya kukaanga na samaki ilivyoshika kasi mitaani jijini Dar, ukiibua uchumi mpya

## • Kitoweo samaki; chanzo cha robo ya protini mwilini • Kwa mwezi, mtu anamla uzito kilo mbili kasoro robo • Mihogo & samaki: Imemwibulia mlalahoi 'lanchi' mpya

**Na Christina Mwakangale**



Wateja wa mihogo na samaki, wakijipatia mlo wa mchana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

ULAJI mihogo hasa kwa mikoa ya ukanda wa Pwani nchini, si jambo la ajabu kwa wakazi wa maeneo hayo

Ni zao linalostawi sana katika ukanda huo na kufanya wakazi wake kutumia katika mlo wa kifungua kinywa asubuhi na hata msimu wa kufunga kwa ajili ya toba na sala. Muhogo mlo muhimu.

Hatua ya maendeleo imepigwa katika muhogo huo. Hivi sasa jijini Dar es Salaam, kuna mtindo mpya wa ulaji mihogo unaoenda sambamba na kitoweo cha samaki pembeni, kuunda 'kufurushi' aina yake.

Ni mlo mahsusi kwa majira muda tofauti wa mahitaji ya mlo jijini; asubuhi, mchana na hata jioni.

Ofisa Lishe kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili -Mloganzila, Theresia Thomas, anasifu jozi ya ulaji mihogo na samaki, una manufaa kwa mlaji iwapo atazingatia kiwango cha nishati kinachotakiwa mwilini kwa siku.

Theresia anaweka angalizo kwamba, kuwapo kipimo cha ulaji mlo huo, kuzingatia mahitaji ya wanga hasa unaopatikana katika muhogo na protini (kutoka katika samaki) inayohitajika kwenye mwili wa binadamu.

**WANAOTEMBEZA JIJINI**

Ndani ya mizunguko jijini, katika vituo vikuu vya usafiri wa daladala na mtaani, ndiko kumetawaliwa na mtindo huo mpya wa maisha jijini.

Wauzaji mihogo na samaki waliokaangwa katika tofauti jijini, wanaelezea namna ambavyo soko la bidhaa zao zimekuza kipato chao, ingawa wanakumbana na vikwazo tofauti kufanikisha malengo.

Maria Abraham, muuza mihogo ya kukaanga katika kituo cha mabasi ya daladala, Stesheni katikati ya jiji, anaiambia Nipashe kwamba alianza biashara hiyo kwa kuuza jirani na nyumbani kwake Kitunda, nje kidogo ya jiji, lakini baadaye alihamishia mjini aliko sasa, katika jiihada za kusaka soko kubwa.

"Nilianza kuuza mihogo ya kiasi cha Sh.5,000 kwa siku nikiwa Kitunda, lakini niliamua kukuza biashara hii kuhamia eneo kuliko na mahitaji.

"Hapa Stesheni ninajumua mihogo ya Sh. 30,000 kwa siku ninauza yote faida, napata mara mbili au tatu, inanisaidia kuitunza familia yangu, mimi ni mjane," anaeleza.

> **"Changamoto huwa napata msimu ambao mihogo inapanda bei, nanunua bei kubwa na siwezi kumpandishia bei mteja, kipande cha muhogo nikikaanga nauza Sh. 200.**

Anabainisha kuwa, ulaji mihogo kwa wateja wake hivi sasa, inakwenda sambamba na ulaji samaki na kwamba inafanya biashara yake kuwa na soko zaidi.

"Samaki mimi siuzi, ila kuna vijana ambao wao wanatembeza samaki aina ya vibua wameshawakaanga wanapitisha hivyo wateja wananunua na mihogo niliyokaanga," anasema Maria.

Anasema uuzaji mihogo umemfanya amudu kuhudumia familia, kununua kiwanja eneo la Chanika, nje ya jiji ingawa anadokeza tatizo adimu la upatikanaji mihogo.

"Changamoto huwa napata msimu ambao mihogo inapanda bei, nanunua bei kubwa na siwezi kumpandishia bei mteja, kipande cha muhogo nikikaanga nauza Sh. 200," anasema.

Hoja hiyo ya kijasiriamali, inamwangukia muuza samaki katika eneo la Posta nako katikati ya jiji, Musa Haji anayeiambia Nipashe kwamba, anasema amefanya biashara hiyo kwa takribani miaka tisa sasa.

Anakiri hivi sasa wateja wa samaki wameongezeka zaidi, ingawa analalamika namna ya upatikanaji kitoweo hicho.



Muuza mihogo ya kukaanga akiandaa bidhaa zake.

"Ninanunua samaki ndoo ndogo kati ya Sh. 60,000 hadi 70,000 kutegemeana na siku. Wakiadimika samaki aina hii ambayo inaliwa zaidi kipindi hiki na mihogo, aina ya kibua, kipindi cha mvua au bahari ikichafuka mawimbi yakiwa makubwa wavuvi hawaendi. Wavuvi wanatumia vifaa duni ambavyo haviwezi kukabiliana na mawimbi makubwa," anasema Musa.

Anasema, siku ambazo ni ngumu kwake kibiashara ni pale panakuwapo ugumu wa kupata malighafi ya samaki, ufukweni Feri kunakouzwa malighafi hayo.

"Sina ujuzi wowote kuhusu hali ya hewa, lakini siku ikiwa ngumu najua tu, utakuta unafika Feri unakuta samaki hamna au wamenunuliwa kwa bei kubwa na wenye fedha, siku nikikosa narudi nyumbani Buguruni na ndoo yangu bila samaki," anasema Mussa.

Pia, anasema katika mazungumzo yao na wavuvi, huwaeleza kuwa majira na kalenda za bahari, wakitambua siku za hatari baharini.

"Hii biashara inanifanya niishi mjini. Nimeoa, nimenunua kiwanja. Kuna changamoto ya mtaji ili niweze kupata eneo maalum, ambalo mteja akinihitaji anajua atanipata wapi.

"Hapa ninatembeza tu katika sinia na kiasi ninachobeba ni kidogo au ambaye amenizoea hasa wa maofisini, anasema niletee samaki nile na mihogo.

"Ningekuwa na kijiwe maalumu, ningekaanga hata samaki ndoo tatu kwa siku wakaisha, watu wanakula sana samaki na mihogo kipindi hiki," anasema Musa.

**WALAJI SAMAKI**

Mmoja wa wateja mla samaki na mihogo, Hamza Seif, mwenye umri wa makamo an amekwishaushi jijini kwa takriban miaka 40, anajitambulisha daima ni mlaji wa mlo huo bila kukosa kila siku, akifafanua:

"Tunaokula labda mihogo ya kukaanga ya shilingi elfu moja na samaki kibua wa shilingi 500 tunapiga 'pasi ndefu (kutokula mchana), hatuna fedha. Mimi nikila hivi nashiba hadi usiku ninaporudi nyumbani.

"Nimeokoa bajeti yangu ambayo ningeitumia kwa kifungua kinywa, chakula cha mchana. Ninatumia shilingi 1,500 tu maji ya kunywa siku imeisha."

Inaelezwa kwamba, ni mlo unaowasaidia wenye uchumi mdogo na kuwapunguzia makali ya gharama ya mlo wa asubuhi na mchana.

**NENO LA SERIKALI**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah (Uvuvi), akifungua maadhimisho ya chakula kitaifa duniani, Oktoba 10 mwaka huu mkoani Njombe anasema, sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama.

Aidha, anasema inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta hiyo ya uvuvi.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, katika bajeti iliyopita ya 2019/20, sekta hiyo imekuwa kwa wastani wa asilimia 1.5 na kuchangia Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 1.71 na anarejea taarifa ya mwaka 2018, ulaji samaki duniani kila mtu mmoja anakula kilo 20.3 kwa mwaka.

Katika hesabu rahisi kila mwezi mtu anakula wastani wa samaki mmoja, mwenye uzito wa kilo mbili kasoro robo.

Shirika la Umoja wa Mataifa Duniani (UN), linasema zaidi ya watu milioni 200 kati ya bilioni moja wakazi barani Afrika, ni walaji wakuu wa samaki, kila mara ni lishe bora ya duniani hususani kwa walioko jirani na mito, pia ufukweni.

**KUTOKA FAO**

Pia Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO), linasema jamii nyingi zikiwamo za wavuvi wanategemea samaki, kwa mlo wa uhakika na ajira na kwamba binadamu wanakula zaidi ya tani milioni 100 za samaki kila mwaka.

Kuna Siku ya Uvuvi Duniani inayoadhimishwa kila Novemba 21 ya mwaka na FAO inaeleza umuhimu wake kwa sekta hiyo, maisha ya binadamu, viumbe majini na mengine ndani na nje ya maji.

Utafiti uliofanywa na FAO karibuni unabainisha wastani wa theluthi mbili ya samaki wote duniani, ama wamevuliwa au wanavuliwa kupita uko wa kiasi kinachotakiwa, sababu kuu zikiwa kutoweka makazi ya samaki, pia uchafuzi na ongezeko la joto duniani.

Inakadiriwa sekta ya uvuvi hususan wavuvi wadogo wadogo, inaajiri asilimia 90 ya watu wanaojihusisha na masuala ya uvuvi, huku asilimia 65 ya uvuaji wote ikifanyika katika nchi zenye kipato cha chini na upungufu wa chakula.

Umoja wa Mataifa (UN) unasema kati ya watu milioni 30 hadi milioni 60 katika nchi zinazoendelea, wanajihusisha na uvuvi kwa mujibu wa FAO, ulaji samaki ni muhimu kutokana na kuwa na zaidi ya asilimia 25 ya virutubisho vya protini katika chakula.

Hata hivyo UN inaonya, zisipochukuliwa hatua madhubuti kukabili athari za uvuvi usio endelevu, kunaweza kusababisha mgogoro mkubwa kutokana na ukosefu wa kitoweo hicho.

FAO hadi sasa inaeleza kufanya uchambuzi na ufuatiliaji wa hali ya kiasi cha samaki duniani, kutokana na kuwapo uchafuzi wa majini, mabadiliko ya hali ya hewa, uharibifu wa makazi ya samaki na kuwapo uvuvi uliopitiliza mipaka.

Msisitizo wa sasa unaangukia kuwapo kiwango endelevu, dhidi ya athari za kibaiolojia inayoshuhudia kupungua kwa samaki kwa kiasi kikubwa.

Malalamiko ya FAO ni katika mazingira yanayozingirwa na ugumu wa kisiasa kusimamia uvuvi katika hali ya viwango vya juu ya umaskini. Kuboresha uvuvi kunategemewa katika kuelewa ukweli wa ikolojia, kijamii na uchumi wa jamii husika.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Maajabu yalivyogubika mwaka 2020






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

KILA mwaka unapomalizika, watu hukaa chini na kutafakari yaliyopita ya mwaka uliopita na kuona walifanya nini na hawakufanya nini, nawajipange vipi kwa mwaka mpya unaoanza.

Wengine hutafakari ni mambo gani yalitokea na kwanini kama ni mema, yaendelezwe na kama ni mabaya, hadhari ichukuliwe yasije irudia katika mwaka unaoanza. Hata hivyo, ilishazoeleka kuwa kila mwanzo wa mwaka, kwa wengi huwa kuna matumizi makubwa yanayouma na pengine pia huchangiwa na matumizi ya mwisho wa mwaka uliotangulia, kutokana na kuendekeza sherehe.

Mimi kwa upande wangu niliamua kutafakari maajabu yaliyonishangaza mwaka jana! Ni mengi, mengine makubwa na mengine madogo, ambayo hayawezi kunishughulisha. Ukiona nayaelezea hapa, ujue yamenishangaza kweli kweli, mpaka nashindwa kuamini.

Nianze na hili la UVIKO-19, wengine wanaopenda Kizungu huita COVID-19. Hivi kwanini nisishangaejinsi UVIKO ulivyopigwa kumbo na Tanzania, mpaka ukarudi Uchinani huko bila hata kuaga!

Utashindwaje kushangaa, wakati dudu hilo limewashinda Wakoloni, Wahisani na Mabeberu wetu hao, sisi kwetu likagonga mwamba na kujiondokea kimya kimya kama lilivyoingia. Hakuna cha barakoa wala sanitaiza.

Hakuna lokidauni wala kujifungia ndani, tunatesa tu mitaani. Mungu ashukuriwe kwa kupokea maombi yetu. Tanzania oyee! JPM oyee!

Lingine lililonishangaza na kunishitua, kwa kweli ni hili lililotokana na Uchaguzi Mkuu tulioufanya Oktoba 28 mwakajana. Kujiandikisha na kuhakiki daftari wala havikunishitua. Kupiga kura, wala hakuniajabisha. Matokeo bhana! Wee acha tu!

Kama wewe hukuajabishwa, basi mimi niliajabishwa na jinsi vigogo wa upinzani walivyopukutishwa na watu ambao hata sikuamini kama ingekuwa hivyo! Kwangu yalikuwa maajabu bin mazingaombwe walahi! Unaona kabisa mtu ambaye ulijua lijejua inye mvua, asingeweza kugalagazwa, lakini ndiye akagalagazwa! Kiboko ilikuwa yale mabao 12-1.

Washangiliaji wooote wale, jamaa kaibuka na kamoja kwa kumina viwili vya mshindi! Sasa njoo majimboni, ah, ah, ah! Watu walipigwa mabao mpaka huruma, watu walishajipanga kushangilia, lakini alipoSimama Waitu Semistokosi, haaa wote chali!

Haikuishia hapo, maajabu mengine, kabla moshi haujatulia na vumbi halijatua, tukasikia dada zetu fulani wanaapishwa kuwa wabunge, tena kwa mara ya kwanza wanaapia nje ya Bunge. Tulipotoa macho ya kuduwaa, Job akaibuka na kusema mlikuwa wapi nyie, kanuni zilishabadilishwa kitambo, si lazima ndani ya Bunge nyie hata nje. Tukajifuta midomo, kuuliza au pande wa walikotoka, tukaambiwa mbona hao sisi hatujawateua kwenda kukalia viti maalumu bungeni, walikotoka haijulikani, hivyo wafungashe virago tu waende wakujuako. Wakitaka wakate rufani, kwetu sisi vyumba tumepangisha. He! Maajabu, sasa walikwenda kwendaje kwa Job? Kitendawili!

Wakati tukisubiri matokeo ya rufani Baraza Kuu la Wadhamini wao, juzi kati hapa nikawa nasikiliza redio, mara nikasikia watangazaji wa kituo kimoja hivi wakimhoji mmoja wa mameya wa moja ya halmashauri za Jiji la Dar es Salaam. Meya aliyechaguliwa hivi karibuni, akiwa amekwenda kuhanikiza ajenda na mipango yake kwenye halmashauri yake.

Kilichonishangaza tena, nikamsikia kwa masikio yangu, akiulizwa eti kwanini kwenye halmashauri yake au wilayani kwake, watu hawana pesa mifukoni? Mtangazaji akasema mbona watu wanaukata sana tatizo ni nini?

Walipomhakikishia kuwa anasikilizwa mbashara, wilayani kwake nchini, duniani na kwenye mitandao ya kijamii, mstahiki akakohoa kidogo na kujibu kwa ukakamavu:

"Zamani hizo pesa walizokuwa nazo zilikuwa za wizi tu, sasa hivi zimebanwa, ndiyo sababu hamzioni."

Nikajiuliza kumbe zile fedha nilizokuwa nalipia wanangu ada zilikuwa za wizi! Maajabu! Alipomaliza hilo, mtangazaji mwingine akachomeka kuhusu machinjio ya kisasa yanavyoendelea na ujenzi na kama yamekamilika, yatasaidiaje.

Kama mwanzo, mstahiki akakohoa kidogo na kujibu:"Tuko hatua nzuri kabisa, na hivi karibuni tutaanza kuchinja na tutauza nyama nje ya nchi.

"Watachinjwa ng'ombe wa madaraja ya chini na ya juu… ya chini nyama mtakula nyie na ya juu nyama itauzwa nje."

Nilikuwa nimejilaza kitandani ikabidi kwa mshangao niinuke, nikakumbuka minofu ya sangara na mapanki ya Mwanza, kwamba minofu Ulaya, mapanki Mwanza! Meyaaa! Alamsiki!

UCHUMI

HIFADHI MPYA MINZIRO

# Chimbuko 1947; misitu, mapango ya vita kuu, inaongoza Afrika kwa vipepeo

• Miaka sita rasmi, ndege wako aina 350 • Ushuhuda wa vifutu wenye mapembe • Vijiji jirani vyatabasamu 'sasa raha tupu'

**Na Lilian Lugakingira,** MISSENYI



Namna wanyama wakiwa ndani ya Hifadhi ya Minziro. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

MARA nyingi inapotajwa mwaka 1947, huwa ina tafsiri ya masihara 'zama zile'. Lakini kwa umri wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Minziro, wilayani Missenyi, ndiyo hasa mwaka wake wa kuzaliwa.

Ni hifadhi yenye wasifu wa kuwa na vipepeo aina nyingi Barani Afrika, ikiwa na ukubwa wa hekta 25,717 chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) na mwaka 2016 ilipandishwa rasmi kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia.

Bernard Mwigulu, ni Mhifadhi wa Minziro, anayesema mchakato wa kupandishwa wa Hifadhi ya Mazingira Asilia, ni mchakato ulioshirikisha wadau mbalimbali, vikiwamo vijiji vinane jirani.

"Lengo kubwa la uhifadhi wa msitu wa Minziro ni kusimamia hifadhi katika kurudisha na kubaki katika uasili wake, kwa hiyo menejimenti inahamasisha matumizi rafiki ikiwa ni pamoja na utalii wa kiikolojia na kiutamaduni," anasema.

Pia anaongeza kuna utafiti unaonyesha Hifadhi ya Minziro, ina aina zaidi ya 600 za vipepeo na ndio hifadhi inayoongoza Afrika.

"Vipepeo ni moja kati vivutio vya utalii, watu hufika kuviona na kupiga picha, vipepeo hawa hupatikana muda wote, lakini mwezi Julai na Agosti ndiyo muda ambao wanaonekana wengi zaidi," anasema.

Anasema, vipepeo hupenda zaidi kwenye mwanga na ndiyo maana katika kipindi cha jua wanapatikana zaidi, hivyo mkakati ulioko ni kuandaa sehemu vipepeo wataonekana kirahisi ili watalii wawafikie.

Pia, anasema Hifadhi ya Minziro ina aina ya ndege zaidi 350, wakiwamo Kwale na Mbayuwayu wa Bluu wanaopatikana katika msituni na wako hatarini kutoweka.

Anavitaja vivutio vingine ni wanyama tembo, nyati, jamii ya nyani kama vile komba na nyoka vifutu wenye mapembe.

Mwigulu anasema, ni hifadhi yenye mimea mbalimbali kama kahawa pori, ambayo ni adimu duniani na miti ambayo magome yake hutumika kutengeneza nguo.

### MAENEO MAALUM

Pia, anataja kuwapo pango la Malila, lililotumika wakati wa Vita Kuu vya Pili vya Dunia na ngome za Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia, katika kilima anachokitaja kwa jina la Bulembe.

Anasema, katika hifadhi hiyo kuna kilima kinachoitwa Kele, ambacho wananchi hukitumia kwa ajili ya matambiko na kupafanya paheshimike.

"Eneo hilo la matambiko linasemekana lina maajabu, mfano husikika sauti ya mtu asiyeonekana. Wananchi hawakatazwi kwenda pale kutambika, kwa kuwa shughuli zao hazina athari kwa msitu," anaeleza.

> **Eneo hilo la matambiko linasemekana lina maajabu, mfano husikika sauti ya mtu asiyeonekana. Wananchi hawakatazwi kwenda pale kutambika, kwa kuwa shughuli zao hazina athari kwa msitu.**

Mwigulu anasema, utalii ni shughuli rafiki wa mazingira, na Hifadhi ya Minziro inaboresha miundombinu na kutangaza utalii wa ndani na nje ya hifadhi, kwa kujengwa kambi inayoendelea kuboreshwa kukidhi mahitaji ya watalii wanaopenda kulala hifadhini.

"Tumetengeneza pia njia za kupita msituni kutembelea vivutio mbalimbali, wakiwamo ndege, wanyama na miti, pia tunaongeza mawe katika mipaka, ili kuepusha migogoro baina ya hifadhi na wananchi tunaopakana nao," anasema.

### HALI YA SOKO

Mhifadhi Mwigulu anasema, jitihada zinazofanyika zinalenga kuongeza idadi ya watalii katika ukanda wa magharibi ambao uko nyuma, akiwa na ufafanuzi:

"Tunatangaza vivutio vya utalii kupitia maonyesho mbalimbali mfano siku kuu ya wakulima (Nanenane), maonyesho ya urithi wetu, pia tunaandaa na kusambaza vipeperushi na machapisho mengine."

Hata hivyo, anakiri sasa utalii katika ukanda wa Magharibi una mabadiliko ya mwamko watu kuifahamu hifadhi hiyo, akitoa mfano mwaka 2015 hapakuwapo mtalii aliyetembelea hifadhi, lakini mwaka 2019 walifika 50 na wanaendelea kujitangaza.

Moja ya jitihada zilizoko ni kuhamasisha utalii wa ndani hasa kwa wananchi wanaoishi jirani na hifadhi, badala ya kutegemea wanaotoka nje ya nchi pekee.

Anasema iliyopo ni kushirikiana na kampuni binafsi za utalii na wadau wengine wakiwamo wamiliki wa hoteli zilizoko mjini Bukoba, kusaidia kuitangaza hifadhi.

"Wamiliki wa hoteli ni muhimu katika masuala ya utalii maana wao ndiyo wanapokea watalii wanaokuja Kagera," anasema mhifadhi huyo.

### URAFIKI NA VIJIJI

Katika ile sera ya kushirikisha wadau wa jirani, Mwigulu anasema katika vijiji vinane wanavyopakana navyo, wanashirikiana na uongozi na wananchi wa vijiji vyote katika utunzaji mazingira kupitia kamati za maliasili za vijiji.

"Kati ya hivyo vijiji vinane, vijiji vitano vinazunguka msitu kwa nje, lakini vijiji vitatu ambavyo ni Karagara, Minziro na Kigazi ambacho kipo mpakani kabisa na nchi ya Uganda, vinazungukwa na msitu" anasema.

Anasema, huko nyuma kamati hizo zilififia na sasa Hifadhi ya Minziro imesaidia kufufuliwa: "Sasa ushirikiano na hifadhi ni mkubwa, maana mbali na wananchi kushiriki kuilinda."

"Pia, wanasaidia kutoa taarifa haraka endapo watabaini uwepo wa watu wanaofanya shughuli hatarishi," anasema Mwigulu, anayesema urafiki huo na vijiji jirani, wakazi vijijini wanaruhusiwa kuchukua kuni kavu siku mbili kwa wiki; Jumatano na Jumamosi.

"Matumizi mengine ni kuchukua dawa za miti shamba ambayo huomba na kuruhusiwa, maana ni matumizi ambayo hayana madhara katika uhifadhi, lakini kukata miti, kuvuna mbao, kuchoma mkaa hawaruhusiwi," anasema.

Emmanuel Joseph, ni mkazi wa kijiji jirani cha Karagara kinachopakana na Msitu wa Minziro, anakiri anafaidika na msitu kwa kuruhusiwa kukusanya kuni kavu.

"Kukata miti haturuhusiwi, lakini kuokota kuni kavu na kuchuma dawa za asili kwa ajili ya kujitibu magonjwa mbalimbali, ikiwamo malaria tunaruhusiwa," anasema.

Joseph anasema, msitu unawafanya wana vijiji jirani kupata mvua za kutosha, zinazowaongeza uzalishaji katika kilimo.

Pia, anasifu elimu wanayoipata kutoka kwa maofisa misitu wa Hifadhi ya Minziro, inawafanya wawe watiifu kulinda hifadhi kwa kuzuia kuchomwa moto na kutoa taarifa haraka, endapo watabaini uharibifu wa aina yoyote.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kigazi, mpakani na nchi ya Uganda, Suleiman Hussein, anasema zipo kamati za mazingira zinazolinda msitu kwa kushirikiana na wananchi na Mamlaka ya Hifadhi ya Minziro.

Hussein anasema katika ushirikiano huo, wananchi wanawapokea watalii na kuwatembeza katika maeneo wanayoyafahamu kushuhudia vivutio hifadhini.

Akieleza uzuri wa msitu huo anasema kuna miti aina ya "Mtoma" ambayo huwapatia anachokiita "mirumba" kwa ajili ya kutengeneza kofia zinazopendwa sana na watalii.

"Wapo wananchi wanaingiza kipato kwa kutengeneza kofia, mashati na mashuka maalumu ambayo hutumika kuwafunga rubega watoto wanapofiwa na wazazi kama baba, ikiwa ni ishara ya kuthibitisha kuwa aliyefungwa shuka hilo ndiye mrithi," anasema.

Mwenyekiti huyo anaziomba mamlaka zinazohusika kuongeza jitihada za kuitangaza hifadhi hiyo, ili kuwezesha watalii waongezeke.

"Watalii wakiongezeka kuja kutembelea vivutio vilivyoko katika hifadhi, kipato chetu wananchi tulioko karibu na hifadhi kitaongezeka, lakini pia serikali itapata mapato kutokana na fedha zitakazolipwa na watalii," anasema.



# Kata 360 kuunganishwa TEHAMA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema ndani ya miaka mitano (2020-2025), serikali itafikia huduma ya mawasiliano katika kata 361 ambazo hazina huduma hiyo kwa sasa.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo juzi alipotembelea Ofisi ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) jijini hapa.

Alisema kwa sasa, mawasiliano yamefikishwa katika vijiji 3,119 kwenye kata 994 na kuwafikia Watanzania milioni 12.2 nchini tangu mfuko huo uanze.

"Tunatarajia katika kipindi hiki cha miaka mitano iliyobaki, kata 361 zilizobaki zinafikiwa kupata mawasiliano ili lengo la Watanzania wote kufikiwa na huduma ya mawasiliano litimie na ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM 2020-2025," alisema.

Aliutaka mfuko huo kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia ilani hiyo pamoja na maelekezo yaliyotolewa na Rais John Magufuli alipokuwa akizindua Bunge mwaka jana.

"Mkajipange upya kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu yenu na kuhakikisha yale maeneo ambayo hayajafikiwa yanafikiwa. Pia, mwongeze ubunifu katika utekelezaji wa majukumu yenu kwa kuangalia teknolojia za gharama rahisi," aliagiza.

Waziri huyo pia aliuagiza mfuko huo kuangalia upya mfumo wa usambazaji wa mawasiliano na kutumia teknolojia za gharama nafuu, ili kufikia maeneo hayo yasiyo na huduma.

Dk. Ndugulile alisema kujenga mnara mmoja wa mawasiliano ni takribani Sh. milioni 350, lakini kuna teknolojia rahisi za gharama nafuu ambapo mawasiliano hayo yatafika katika maeneo hayo ya pembezoni.

"Lengo ni kuhakikisha gharama za mawasiliano zinaendelea kushuka ndani ya nchi yetu na kuongeza wigo wa watumiaji ili kufikia Tanzania ya uchumi wa kidigitali, na mfuko huu una mchango mkubwa sana katika malengo hayo makuu ya kuhakikisha Tanzania ya digitali inafikiwa," alisema.

Dk. Ndugulile alisema ni lazima kuendana na kasi hiyo na kuondokana na sheria za zamani zisizoendana na hali ya sasa.

"Hatuwezi kuwa na sheria inayosema duka lina kuta nne, lina leseni na vibali vya biashara, duka linaweza kuwa sehemu yeyote, duka hili ni mawasiliano lazima tuendane na kasi ya kidunia na kuwa na mifumo na sheria zinazoendana na kasi hiyo hiyo," alisema.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, aliahidi kufanyia kazi maagizo ya waziri huyo ili kuendana na hali ya sasa.



Wauza mboga wa soko la Sabasaba jijini Dodoma wakifanya biashara kwenye eneo linalohifadhiwa takataka bila kujali afya zao na wateja. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Magereza yajitosa huduma za ulinzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza nchini limeanza kutoa huduma ya ulinzi katika taasisi za umma na kampuni binafsi kama ilivyo kwa kampuni nyingine za ulinzi nchini.

Huduma hizo zinatolewa kupitia Shirika la Magereza (SHIMA) ambalo ndani yake, limeanzisha huduma ya ulinzi kupitia kampuni yake ya Shima Guard. Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shima Guard, ACP Abdalah Msepwa, alisema jeshi hilo linatumia vijana ambao wamehitimu mafunzo ya uaskari yaliyotolewa na jeshi hilo hivi karibuni, lengo likiwa ni kuwaweka sawa kabla ya kuanza kazi hiyo.

"Tunatarajia kuanza kutoa huduma hiyo haraka iwezekanavyo. Tayari tuna askari 97 ambao wamehitimu mwaka huu mafunzo hayo," alisema ACP Msepwa.

Alibainisha kuwa tayari wamepeleka maombi kwenye taasisi na kampuni ili kutoa huduma hiyo huku akisema wana mpango wa kupanua huduma hiyo hadi kwa watu binafsi.

Msemaji wa Jeshi hilo, Amina Kavirondo, alisema mradi wa kampuni ya ulinzi unaotekelezwa ni moja ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi hilo kupitia shirika lake hilo ambalo linafanya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kavirondo aliitaja baadhi ya miradi ambayo shirika hilo linatekeleza ni pamoja na ujenzi, kilimo, utengenezaji wa samani na wa ulinzi ambao unatekelezwa na Shima Guard.

Alisema mradi wa ulinzi umeanza hatua ya kwanza lakini kadri siku zinavyokwenda, utaendelea kutekelezwa kwa sehemu kubwa kulingana na matarajio ambayo jeshi limejiwekea.

"Huu ni mwanzo tu wa Jeshi la Magereza kutekeleza miradi mbalimbali, kuna miradi mingine mingi inakuja jamii ijiandae kuipokea," alisema Kavilondo.

Kavirondo alisema jeshi hilo limejipanga kutoa huduma bora ya mradi huo wa ulinzi kutokana na kwamba vijana wamepatiwa mafunzo ya kutosha kutoka kwa jeshi hilo.

## Waziri: Hatutacheka na walaji fedha za ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeapa kutocheka na mtu yeyote atakayebainika kuchezea fedha za ushirika ili kurudisha hadhi na heshima ya ushirika.

Pia, inatarajia kuitisha mkutano wa wadau wa ushirika ili kupitia upya Sheria ya Ushirika iliyopo iendane na mahitaji ya sasa.

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa katika hafla ya kukabidhi magari matano na kompyuta 70 kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi kwa watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC).

Alisema bado kunahitajika mapambano dhidi ya wizi na ubadhirifu kwenye vyama vya ushirika licha ya kuonekana kupungua kutokana na jitihada zilizofanywa na serikali za kurudisha mali za ushirika.

"Siyo kwamba ushirika wa zamani ulipofanikiwa hakukuwa na wizi au ubadhirifu, hapana ila kuna kipindi hapa katikati ulikubuhu sana, mali za ushirika zinapotea, hazifahamiki zilipo.

"Tuna kesi moja TRA (Mamlaka ya Mapato) inadai fedha ushirika kwa kitu ambacho ni mzabuni ndiye aliyepaswa kulipa kodi.

"Sasa unatafuta kwenye kumbukumbu za ushirika humuoni huyo mzabuni. Kwa hiyo, deni linaenda kwenye chama cha ushirika na ni mzigo kwa wakulima, hii ni njaa kufanya mchezo na kuongeza mzigo kwenye ushirika.

"Hatutachekeana na mtu anayecheza na mali za ushirika, kwa sababu ukifanya hivyo, unakatisha watu tamaa, watakuwa hawana hamu ya kujiunga na ushirika. Warajis Wasaidizi tusimame kidete kwenye hilo," aliagiza.

Alisema kuwa licha ya ubadhirifu kupungua, bado kuna tatizo la vyama kushindwa kuandaa vyema hesabu zake na kusababisha kukosa hati safi.

Alinukuu ripoti ya ukaguzi wa vyama vya ushirika 43 iliyofanywa na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kwa mwaka 2019/20, inayoonyesha hakuna chama kilichopata hati safi.

"Kuna kazi kubwa ya kujenga uwezo, kuna ripoti ya COASCO, ukiisoma inaonekana mbaya sana, lakini kwa kiasi fulani inaonyesha ni udhaifu, hakuna mhasibu mzuri anayeweza kuandaa vitabu vya hesabu ambavyo vitakaguliwa," alisema.

Vilevile, alisema ripoti hiyo inaonyesha kuna tatizo la kutoweka vizuri kumbukumbu na kwa uchache kuna wizi na ubadhirifu.

"Kwa hiyo, tusipojenga uwezo, hizi kumbukumbu na kuendelea kupata hati ambazo siyo nzuri, watu watakata tamaa, pia kwa upande wa AMCOS, 3,374 zilizokaguliwa, hati safi 34, zenye shaka 169, zisizoridhisha zipo 605 na hati mbaya zipo 1,045, kuna kazi kubwa," alisema.

Aliahidi kutumia taarifa hiyo kushughulikia udhaifu uliobainika ili kuleta ufanisi kwenye ushirika.

Kuhusu sheria, waziri huyo alisema kuna kazi ya kurudisha imani za watu kwenye ushirika kwa kupitia upya Sheria ya Ushirika na tayari kazi imeshaanza.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo ambaye ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, alisema tume itaendelea kupambana na kero zinazoukabili ushirika ikiwamo ubadhirifu na uongozi mbovu kwenye vyama hivyo.

Dk. Ndiege alisema tume ipo kwenye mpango wa kuimarisha ofisi za ushirika nchini ni itahakikisha kila mkoa una gari kabla ya mwaka wa fedha 2020/21 kufika ukomo.





## Bilioni 3.5/- zahitajika kutatua shida ya maji

**Na Mwandishi Wetu**

SHILINGI bilioni 3.5 zinahitajika kwa ajili ya kutatua tatizo la uhaba wa maji katika miji ya Kyela na Kasumulu wilayani Kyela mkoani Mbeya.

Wakazi wa miji hiyo wamekuwa wakihangaika kupata huduma hiyo kutokana na kukosa chanzo cha uhakika cha maji ya kutosheleza miji hiyo ambayo ina watu wengi na imekuwa ikikumbwa na magonjwa yanayotokana na matumizi ya maji machafu.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA), imefanya utafiti na kufanikiwa kupata chanzo kipya cha maji kwa ajili ya kuipatia maji miji chanzo hicho kinapatikana ndani ya Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mbeya-WSSA, Ndele Mengo, alisema chanzo hicho ni cha uhakika na kina uwezo wa kuhudumia miji hiyo na vijiji vinavyozunguka chanzo hicho.

Alisema kwa sasa wanatafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo na wakipata fedha hizo, wataukamilisha mradi huo ndani ya miezi 18 na wananchi kuanza kupata huduma.

"Haya maji ni safi na ni mengi sana, chanzo kipo na kilishajengwa miaka kadhaa iliyopita na sasa hivi kinahitajika tu kuboreshwa na kuanza kupeleka maji kwa wananchi," alisema Mengo.

Alisema walishafanya usanifu na kujiridhisha kuwa chanzo hicho kinakidhi mahitaji ya wananchi wa miji hiyo miwili kwa miaka zaidi ya 20 na kwamba wataendelea kutafuta vyanzo vingine ijayo.

Mbunge wa Kyela, Ally Mlaghila, alisema mradi huo ni muhimu kwa ajili ya kukabili tatizo la maji kwenye jimbo hilo kwa maelezo kuwa tatizo kubwa la wilaya hiyo ni maji.

Alisema wananchi wamekuwa wakitumia muda mrefu kutafuta huduma hiyo kwenye mito na visima ambavyo wakati mwingine usalama wake unakuwa siyo wa uhakika kutokana kuwa na uwezekano wa kuwa na vimelea.

"Sisi wana Kyela tatizo kubwa linalotukabili ni maji, tunawaomba watu wa mamlaka mtusaidie kukamilisha mradi huu mapema ili tuondokane na tatizo hili," alisema Mlaghila.

Baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kyela, walisema wamekuwa wakikumbwa na magonjwa ya kuhara na kushambuliwa kwa mfumo wa mkojo (U.T.I) kutokana na maji wanayotumia kuwa na vijidudu.

# Ashikiliwa polisi tuhuma kuingiza pombe za viroba

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia mtu mmoja kwa tuhuma za kuingiza nchini zaidi ya chupa 390 za pombe kali za aina mbalimbali zilizopigwa marufuku nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Jerome Ngowi, alimtaja mtuhumiwa huyo kuwa ni Christopher Ndomba (42), mkazi wa Wilaya ya Kyela.

Alisema mtuhumiwa huyp alikamatwa Januari 5 mwaka huu majira ya saa 11 alfajiri akidaiwa kusafirisha pombe hizo kutoka nchi jirani ya Malawi kuviingiza nchini kwa ajili ya kuviuza.

Alizitaja aina ya pombe hizo ambazo zimepigwa marufuku kuwa ni WIN chupa 80, Right Choice chupa 120 na Ice Dry London Gin chupa 190 ambazo zote zinatengenezwa Malawi.

Alisema mtuhumiwa alikuwa anasafirisha pombe hizo kwa kutumia pikipiki aina ya Kinglion yenye namba za usajili MC. 793 CQC.

"Hizi pombe zilipigwa marufuku nchini kwa sababu zina kilevi kinachozidia asilimia 41, huyu mfanyabiashara alikuwa amezihifadhi pombe hizo kwenye maboksi matatu kulingana na aina ya pombe yenyewe," alisema Kamanda Ngowi.

Aliongeza kuwa upelelezi wa tukio hilo unaendelea kufanyika na ukikamilika, mfanyabiashara huyo atafikishwa mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Aliwataka wananchi hasa wanaoishi maeneo ya mipakani kuacha kufanya biashara haramu, akionya kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufungwa jela.

Kamanda Ngowi alisema jeshi hilo linaendelea kufanya doria mbalimbali kwenye mpaka wa Kasumulu wilayani Kyela pamoja na maeneo ya kwenye vipenyo visivyokuwa rasmi ili kudhibiti biashara hizo za magendo.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kukomesha vitendo vya uhalifu kwa kutoa taarifa za siri zitakazofanikisha kukamatwa kwa wahalifu ama kuzima uhalifu kabla haujaleta madhara kwenye jamii.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akikagua kiwanda cha kushona nguo cha Jeshi la Magereza katika Gereza la Ruanda jijini Mbeya alipofanya ziara ya kukagua miradi ya jeshi hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijana wanolewa matumizi ya viuatilifu

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Viuatilifu Tanzania (TPRI) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo, imeanza kutoa mafunzo maalum kwa vijana katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu kwenye mashamba, ili kuwasaidia kuepuka madhara ya kiafya.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa jijini Mbeya juzi, vijana wakifundishwa matumizi ya viuatilifu vya aina mbalimbali, vifaa vya kutumia kupuliza na namna ya kujikinga na madhara ya viuatilifu hivyo wakati wa kuvitumia na baada ya kuvitumia.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo kwa vijana zaidi ya 40 wa mikoa hiyo, Mtafiti wa Visumbufu Mimea kutoa TPRI, Ramadhan Kilewa, alisema wameamua kutoa mafunzo hayo kwa vijana hao baada ya kubaini kuwa mfumo wa awali wa utoaji elimu haukidhi mahitaji.

Kilewa alisema kuwa awali walikuwa wanatoa mafunzo hayo kwa wafanyabiashara wa maduka ya viuatilifu ili na wao waifikishe elimu hiyo kwa wakulima wanaokwenda kununua viuatilifu, lakini wamebaini elimu hiyo haitoshi.

"Hawa vijana tunawafundisha ili wao ndiyo wakafanye kazi ya kupuliza dawa hizi kwenye mashamba ya wakulima kitaalamu, lengo letu ni kuepusha madhara ya viuatilifu kwa viumbe visivyolengwa kwenye upuliziaji," alisema Kilewa.

Alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wakitumia viuatilifu bila kufuata maelekezo, kitu ambacho kinaweza kuhatarisha maisha yao na mifugo kutokana na kutokuwa na elimu sahihi ya utekelezaji wa chupa za viuatilifu.

Waandaaji wa mafunzo hayo ambao ni Kampuni ya Corteva inayojihusisha na uzalishaji wa mbegu za kilimo, walisema pamoja na kufundisha matumizi sahihi ya viuatilifu, pia wanalenga kuzalisha ajira kwa vijana.

Mwakilishi wa Kampuni hiyo, Cosmas Maganga, alisema mafunzo hayo yatasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana hao kwa maelezo kuwa watautumia ujuzi walioupata kufanya kazi za kujiajiri na hivyo kujiingizia kipato.

"Kuna baadhi ya vijana hawa walikuwa wanafanya kazi hizo, lakini walikuwa hawana ujuzi, sasa tunawapa mbinu za kitaalamu ambazo zitawasaidia kuboresha kazi zao na ninawashauri wakulima kwenye maeneo yao wakawatumie vijana hawa watawasaidia," alisema Maganga.

Baadhi ya vijana waliopata mafunzo hayo walisema yatawasaidia kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu na kuleta tija kwenye uzalishaji wa mazao shambani.

Mmoja wa vijana hao, Enock Kasisi, ambaye ni mkazi wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, alisema wakulima wengi walikuwa wanatumia viuatilifu hivyo kwa mazoea, hivyo kutopata tija.

Alisema wakulima wengi huwa wanaamini kuwa viuatilifu hivyo huwa vina madhara kwa binadamu na wanyama wengine endapo tu watavimeza, lakini kwenye mafunzo hayo walielekezwa kuwa hata vikigusana na ngozi vinaleta madhara.





Rais mstaafu wa awamu ya saba, Dk. Ali Mohamed Shein, akitoa hotuba katika ufunguzi wa Chuo cha Utalii Maruhubi Wilaya ya Mjini Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Ikiwa ni shamra shamra za miaka 57 ya Mapinduzi Zanzibar. **PICHA: HAWA ABDALLAH**

# SMZ kuimarisha Bandari ya Shumba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema serikali inakusudia kuimarisha Bandari ya Shumba ili kuondoa matatizo yaliyopo na kuimarisha uhusiano kati ya wananchi wa Mombasa na Zanzibar.

Hemed alisema hayo jana wakati akizungumza na wawakilishi wa wananchi wa Kaunti ya Kwale, Mombasa nchini Kenya waliofika ofisini kwake, Vuga, kwa ajili ya kujitambulisha na kumsalimia.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendeleza ushirikiano wake na Kenya katika sekta za afya, kilimo, utalii na uchumi wa buluu ambazo zimepewa kipaumbele na serikali chini ya uongoz wa Rais Dk. Hussein Mwinyi.

Hemed alisema kwa vile Zanzibar ni nchi ya visiwa, imeshaamua kujikita zaidi katika kuimarisha uchumi wa buluu kupitia bahari kutokana na sekta hiyo kuwagusa wananchi wengi sambamba na kuzitumia vyema rasilimali zinazopatikana. Alisema serikali ya awamu ya nane ya Zanzibar imeweka mkazo zaidi katika kuwafikishia huduma muhimu wananchi wake hasa kuinua hali zao za maisha, kitendo kitakachowasaidia kuwaingizia kipato cha kujikimu.

Kuhusu ulinzi na usalama, Hemed aliwataka viongozi hao kuendelea kuwakumbusha wananchi wao kufuata sheria na taratibu kwa kuzingatia nidhamu za uingiaji na utokaji.

Akitoa shukrani zake kwa niaba ya msafara huo, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kupitia Kaunti ya Kwale, Mwepupheh Ndoro, alimweleza Hemed kuwa Kwale imevutiwa na muundo wa SMZ na sasa wako mbioni kurekebisha mfumo na muundo wao ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mwepupheh alimthibitishia Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba Kaunti yake itaendelea kushirikiana na SMZ kupitia Baraza la Wawakilishi Zanzibar katika kuona uhusiano wa pande hizo mbili unazidi kuimarika.

Kaunti ya Kwale, Mombasa, nchini Kenya imekuwa na ushirikiano na Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi Zanzibar takriban kwa miongo mitatu sasa.

# Mwinyi awakumbusha viongozi CCM wajibu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewakumbusha viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wajibu wa kurudi kwa wananchi kuwatumikia na kushirikiana nao katika kuzitafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi katika ufunguzi wa Kongamano la Jumuiya za CCM za UWT, Wazazi pamoja UVCCM lililofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdulwakil, Kikwajuni jijini hapa, likiwa na lengo la kuwapongeza Rais John Pombe Magufuli na yeye mwenyewe kwa ushindi mkubwa waliopata katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba, mwaka jana.

Alisema wananchi wana shida mbalimbali zinazohitaji misaada kutoka kwa viongozi, hivyo akawataka kutokuwasahau wale waliowachagua na kubainisha kuwa huo ndio mwelekeo sahihi wa viongozi wanaotoka CCM.

Alisema uchaguzi umemalizika, hivyo kazi kubwa iliyoko mbele ya viongozi wa chama hicho ni kuwatumikia wananchi kwa kuyatekeleza mambo mbalimbali waliyoyaahidi katika kampeni na kuitekeleza Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya 2020 - 2025.

Pia aliwakumbusha wanachama wa CCM wajibu walio nao katika kujiandaa na uchaguzi ndani ya chama ifikapo mwakani, hivyo akawataka kujiandaa kwa msingi kuwa hatua hiyo itatoa fursa ya kupanga safu za uongozi katika chama hicho. "Nasaha zangu kwenu wakati utakapofika, wachagueni viongozi wenye mapenzi ya dhati na CCM na sio wanaotafuta maslahi yao wenyewe kupitia CCM", alisema.

Dk. Mwinyi alisema hatua zilizoanza kuchukuliwa katika kupambana na ubadhirifu wa mali ya umma, uzembe na ukiukwaji wa sheria pamoja na rushwa, zinalenga kuleta nidhamu katika matumzi ya fedha za serikali.

"Serikali imeanza kuchukua hatua za kupambana na vitendo vya ubadhirifu wa mali ya umma, uzembe, ukiukwaji wa sheria, pamoja na rushwa miongoni mwa watendaji wake kwa dhamira njema ya kuleta nidhamu katika matumizi ya fedha za serikali kwa manufaa ya wananchi," alisema.

Pia aliwahakikishia wana CCM kuwa wale wote watakaohusika na matukio ya vitendo hivyo, watachukuliwa hatua za kisheria bila kumwonea mtu, hivyo akawataka wananchi kuunga mkono hatua hiyo. Akigusia maudhui ya kongamano hilo, Dk. Mwinyi ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, alisema ushindi mkubwa uliokipata chama hicho katika uchaguzi mkuu, ni kielelezo cha imani na matumaini waliyonayo Watanzania kwa chama chao.

Alisema Watanzania wanaridhishwa na utendaji wa chama hicho ndiyo maana wakafanya uamuzi kuendelea kukichagua kwa kura nyingi. Dk. Mwinyi alitoa shukrani kwa viongozi na wanachama wa jumuiya hizo kwa uamuzi wa kuandaa kongamano hilo lenye lengo la kumpongeza kutokana na ushindi mkubwa wa asilimia 76.27 aliopata katika uchaguzi mkuu pamoja na kuipongeza CCM kwa kuwa na utaratibu mzuri wa kidemokrasia wa kupata viongozi katika ngazi mbali mbali.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadalla 'Mabodi', alisema chama kinaunga mkono hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Dk. Mwinyi katika kuimarisha ustawi wa jamii na mapambano dhidi ya udhalilishaji, sambamba na hatua ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Alisema hatua ya kuunda SUK itaendeleza umoja na mshikamano wa Wazanzibari na kudumisha utawala bora.

## Shein ataka mafunzo yafanywe kwa vitendo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, amesema umefika wakati wa kufanya mabadiliko ya kutolewa mafunzo yatayoendana na wakati ili kupanua wigo wa soko la ajira nchini.

Alisema hayo jana katika ufunguzi wa jengo la Chuo cha Utalii Maruhubi jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra ya kutimiza miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Dk. Shein amesema imefika wakati kwa wanafunzi wanaosoma chuo cha utalii kupatiwa mafunzo yanayoendana na wakati ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya utalii.

Aliwashauri wanafunzi wa chuo hicho kusoma kada tofauti za sekta ya utalii ambayo imekuwa tegemeo kubwa la vijana wengi kupata ajira hivi sasa nchini.

Pia Dk. Shein alisema ni vyema kuzalishwa vijana wenye taaluma stahiki kwa kuendelezwa vivutio vilivyopo kwa kufuatwa mila, silka na utamaduni wa nchi na kwamba maendeleo yanayopatikana yanatokana na kuwapo kwa vyanzo tofauti vya utalii zikiwamo hoteli zenye sifa.

Awali, Waziri wa Elimu wa Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, aliahidi kuendelea kutafuta masomo wafanyakazi wa Chuo cha Utalii katika nchi tofauti ili vijana watumie fursa ya kwenda kujifunza kuendesha harakati za kiutalii kiutaalamu zaidi.

Waziri alisema sekta ya utalii imekuwa ikichangia pato kubwa kwa nchi, hivyo kufanya hivyo kutaweza kuwapatia nafasi zaidi za ajira vijana.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idrisa Muslim Hijja, alisema lengo la ujenzi huo ni kuzalisha wataalamu ili kuongeza nafasi za ajira kwa vijana katika kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

Jengo hilo la ghorofa mbili lenye madarasa matano na vyumba tisa vya kulala, limegharimu Sh. bilioni 5.66 na ujenzi wake umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MULEBA MKOA KAGERA**
**MAOMBI NA. 68/2020**

**WAZALENDO SAVING & CREDIT CO-OPERATIVE……….......... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**JOVIN MAKAMULO MAJULA**
……………………….........................
**MJIBU MAOMBI**
**KWA**
**JOVIN MAKAMULO MAJULA**
**(POPOTE PALE ULIPO )**

Unaarifu kuwa maombi Na 68/2020 yamepangwa kutawa tarehe 23.02.2021 mbele ya mwenyekiti wa Baraza , J.K Banturaki saa 2:30 asubuhi , mahali Muleba (Mamlaka ya mji mdogo).
Hivyo, unaamriwa kuhudhuria mwenyewe / mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhulia Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 04.01.2021
………………..

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MULEBA**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MULEBA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JAPHET MARCO MLOLO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 901 ATC** SUBARU FORESTER. Chassis namba **SF5046788.** Engine namba **EJ20215825.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI: MWA/NY/RB/878271/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JEREMIA HENRY MSUYA** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALTEZZA** yenye namba za usajili **T 397 CJF** rangi ya **SILVER** chasis namba **GXE10012023I** engine namba **IGEAA023I,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **CONTROL NO.9910820050302**
Namba ya simu. **0784990934**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BEATRICE MICHAEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1369/0004** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MKALAMO SEKONDARI** mwaka 2006. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya Polisi: KOR/RB/835/09.**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Wafariki wakipinga Biden kutangazwa rais

**Washington,** MAREKANI

POLISI nchini Marekani, imethibitisha kuwa mwanamke mmoja aliyepigwa risasi wakati wa vurugu zilizotokea baada ya wafuasi wa Rais Donald Trump kuvamia bunge, amefariki dunia.

Tukio limetokea huku Bunge la Congres likimwidhinisha, Joe Biden na Kamala Hariss kama rais mtarajiwa na makamu wake nchini Marekani.

Bunge hilo liliwaidhinisha wawili hao kwa kura 282 huku wabunge 138 wakipiga kura ya kupinga matokeo ya jimbo la Pennsylvania.

Bunge la seneta lilikataa pingamizi kama hilo.

Kura za wajumbe zilithibtishwa baada ya mabunge yote mawili lile la uwakilishi na lile la seneta kukataa pingamizi kuhusu kura zilizopigwa katika vituo vya Jimbo la Pennsylvania na Arizona.

Inadaiwa kifo cha mwanamke huyo, kilisababishwa na majeraha aliyopata, huku maofisa wakidai hawajataja jina la mwanamke huyo na kwamba ni raia wa kawaida.

**Wafuasi wa Trump, waliokuwa na hasira waliandamana huku wakiimba, 'Tunamtaka Trump' na mmoja wao akipigwa picha akiwa ameketi kwenye kiti cha rais wa bunge la Seneti.**

Waandamanaji ambao ni wafuasi wa Rais Trump, walivamia jengo hilo jana jioni kulalamika dhidi ya utaratibu wa kuidhinisha ushindi wa Joe Biden. Aidha, mtu mwingine alipigwa risasi katika vurugu hizo, kulingana na Shirika la habari la Associated Press (AP).

Lindsay Watts, mwanahabari wa shirika lenye kuhusishwa na Fox News, aliandika ujumbe kwenye Twitter kuwa, wahudumu wa afya wa Washington DC, walisema juhudi za kumwokoa mwanamke aliye na hali mahututi, zinaendelea baada ya kupigwa risasi kifuani.

Wafuasi wa Trump, waliokuwa na hasira waliandamana huku wakiimba, 'Tunamtaka Trump' na mmoja wao akipigwa picha akiwa ameketi kwenye kiti cha rais wa bunge la Seneti.

Polisi Washington, imesema kuwa ni wazi waandamanaji hao walikuwa tayari kutumia nguvu yoyote ile kuingia katika majengo ya bunge.

Inasemekana hadi kufikia jana watu 13 na silaha tano zilinaswa na polisi wakati ghasia zinaendelea bungeni.

Mkuu wa Polisi, Robert Contee, aliwaambia waandishi wa habari kuwa, waliokamatwa sio wakazi wa eneo la DC. Kuna taarifa kuwa watu walitumia bunduki kwenye jengo hilo, pia mabomu ya kutoa machozi yametumika kutawanya waandamanaji.

Amri ya kutotoka nje imetangazwa baada ya saa 12:00 jioni nchini humo, kutokana na vurugu zilizotokea Washington.

Awali kikao hicho cha kumpitisha Joe Biden, kama rais wa nchi hiyo, kilisitishwa na Makamu wa Rais, Mike Pence, huku akitolewa nje ya jengo.

Polisi waliingilia kati na mabomu ya machozi kwa waandamanaji wanaojaribu kuingia kwenye jengo la Congress.

Rais Donald Trump kupitia mitandao ya kijamii aliwataka waandamanaji "kubaki na amani".

Amri ya kutotoka nje ilitangazwa katika mji mkuu kufuatia matukio hayo.

Trump, katika taarifa yake kabla ya maandamano hayo, alisema kwamba hawatakubali kushindwa na kwamba alishinda katika uchaguzi wa rais uliofanyika Novemba, mwaka jana.

Trump alisema kuwa yeye ndiye mshindi wa kweli wa uchaguzi huo: "Sitakubali kushindwa kamwe, sitaacha."

Mdemocrat Jon Ossoff alipata ushindi katika duru ya pili ya uchaguzi jimbo la Georgia na kuwapa Wademocrat udhibiti wa Baraza la Seneta la Marekani. Mchungaji Raphael Warnock alitangazwa mshindi wa uchaguzi wa pili wa Seneta katika Jimbo la Georgia, Jumanne, wiki hii.

Kinyang'anyiro kati ya Ossoff na Seneta Mrepublican, David Perdue ulikuwa na ushindani wa karibu kabla ya kutangazwa kwa siku nzima.

Ossoff, msaidizi wa zamani wa bungeni na mtengenezaji wa makala ya televisheni, alijitangazia ushindi mapema Jumatano, lakini wakati huo kura zilikuwa zimekaribiana kwa yeyote kutangaza ushindi. **BBC/TRT/VOA**

## Kim Jong Un akiri mpango kiuchumi mwaka 2016 ulifeli

**Pyongyang,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un, amekubali kuwa mpango wake wa kiuchumi wa miaka mitano kwa nchi hiyo ambayo imejitenga, ulishindwa kufikia malengo yaliyowekwa katika kila sekta.

Alikuwa akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao cha dharura cha chama chake cha Workers' Party, ambacho ni cha nane katika historia ya nchi hiyo. Korea Kaskazini, ilifunga mipaka yake Januari, mwaka jana, kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona licha ya madai kwamba, hakujawahi kuwa na maambukizi ya virusi hivyo nchini humo.

Hatua hiyo imesababisha kujitenga na majirani zake ambayo pia ni washirika wake wa karibu, ikiwamo China. Biashara kati ya nchi hizo mbili, imedorora kwa asilimia 80.

Aidha, kimbunga na mafuriko pia vimesababisha nyumba na mazao kuharibika Korea Kaskazini ambayo bado imewekewa vikwazo vikali vya kimataifa, ikiwamo mpango wake wa nyuklia.

Kim, sio jambo la kawaida kukubali makosa yake hatua ambayo imekuwa kama utambulisho wake alisema, Laura Bicker mwandishi wa habari wa BBC mjini Seoul.

Taarifa kupitia televisheni ilionyesha wakiwa kwenye mkutano katika mji mkuu wa Pyongyang, uliokuwa umejaa maelfu ya wanachama na hakuna ambaye alikuwa amevaa barakoa walipokuwa wamesimama kupiga makofi wakimkaribisha wakati anaingia. **BBC**




Wafuasi wa Rais Donald Trump wakiwa wamekusanyika mbele ya jengo la Capitol, jana, wakati Bunge la Congres likimwidhinisha Joe Biden na Kamala Hariss kama rais mtarajiwa na makamu wake nchini Marekani.
**PICHA: REUTERS**

## Mahakama yatupilia mbali dhamana mwanzilishi mtandao wa WikiLeaks

**London,** UINGEREZA

MAHAKAMA ya Uingereza imekataa ombi la kumwachilia huru Assange, kwa dhamana.

Mahakama imekataa ombi hilo la mwanzilishi wa WikiLeaks, Julian Assange, ili kuachiliwa kwa dhamana.

Kesi ya Assange, iliyosikilizwa katika mji mkuu wa London, Jaji Vanessa Baraitser aliashiria kuwapo uwezekano wa mwanzilishi WikiLeaks, kutokuja kwenye usikilizaji wa rufani, ikiwa ataachiliwa huru.

Siku mbili zilizopita, mahakama hiyo ilikataa ombi la Assange kurejeshwa Marekani.

WikiLeaks ambayo ilianzishwa na Assange, ilichapisha nyaraka kadhaa za siri mwaka 2010 pamoja na ushahidi wa uhalifu uliofanywa na Marekani katika nchi za Iraq na Afghanistan.

Assange ambaye alikimbilia kwenye Ubalozi wa London nchini Ecuador, ili asirejeshwe Marekani, alikamatwa na vikosi vya usalama vya Uingereza baada ya kuishi huko kwa miaka 7 na akawekwa gerezani. **TRT**

# SANTO ASHUSHIWA RUNGU EPL




**LONDON,** England

KOCHA wa Klabu ya Wolves, Nuno Espirito Santo amekutana na adhabu ya pauni 25,000 baada ya kumkosoa mwamuzi, Lee Mason katika mechi ambayo timu yake ilipoteza mbele ya Burnley.

Adhabu hiyo imetolewa na Chama cha Soka cha England (FA), baada ya kumtaka kocha huyo aombe radhi, lakini alikataa akiamini alichokisema ni sahihi.

Mchezo baina ya Burnley wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Wolves ulichezwa Desemba 21, mwaka jana ambapo baada ya mtanange huo, Nuno alisema mwamuzi hakuwa na uwezo wa kuchezesha mchezo ule.

Kocha huyo mbali na adhabu hiyo amepewa tahadhari juu ya vitendo vya utovu wa nidhamu kwa siku za mbeleni.

Kwa mujibu wa kanuni za FA, maoni yanayopingana na uwezo hafifu kwa waamuzi yanaruhusiwa, lakini yakibainika kuwa yalikosa usawa na utu adhabu hufuata kwa nyuma, ingawa huwa na sehemu ya kukata rufani.

# Shevchenko atajwa kumrithi Lampard

**LONDON,** England

BAADA ya kufanya vibaya katika mechi tano zilizopita tetesi zinasema kwamba, nyota wa zamani wa Chelsea, Andy Shevchenko anatajwa kuchukua mikoba ya Frank Lampard endapo kocha huyo ataondoka klabuni hapo.

Mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovic, anaangalia orodha ya makocha wanaoweza kuchukua nafasi hiyo baada ya Lampard kufanya vibaya katika mechi kadhaa zilizopita.


Chelsea wamepoteza mechi nne kati ya sita walizocheza kwenye Ligi Kuu England na kuanza kujiuliza kuhusu uwezo wa Lampard kuiongoza timu hiyo baada ya kutumia kiasi cha pauni milioni 200 kweye usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa jarida la Le10Sports, Abramovic anamwangalia Shevchenko kama mrithi wa Lampard.

Lakini Lampard anatarajiwa kuongezewa muda kulingana na ripoti japokuwa kumekuwa na presha kubwa sana kwake.

Shevchenko ni rafiki mzuri wa Abramovic, mtoto wake anacheza katika akademi ya Chelsea na ameisaidia Timu ya Taifa ya Ukraine kucheza katika mashindano ya Euro 2020 inayofanyika mwaka huu 2021.






# *Solskjaer ampa matumaini Van de Beek*

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema, Donny van de Beek ataweza kurejea na kuwa bora zaidi klabuni hapo licha ya kukumbwa na mwanzo mgumu klabuni hapo Old Trafford.

Nyota huyo alitua United msimu wa joto ulipita akitokea Ajax, lakini kwa kiasi kikubwa amekuwa akihangaika kurejea kwenye kiwango chake, baada ya kuchangia goli moja tu katika mechi zale 19 za michuano yote alizocheza hadi sasa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, raia wa Uholanzi bado hajaweza kucheza mechi yoyote ya Ligi Kuu England tangu Desemba 20, mwaka jana na alikuwa benchi bila kutumika kwenye mechi dhidi ya Leicester City, Wolverhampton Wanderers na Aston Villa.

Lakini Solskjaer anaona nyota huyo ataweza kukua zaidi na zaidi akiamua kutulia klabuni hapo.

"Donny ameweza kucheza vizuri pale alipokuwa na nafasi. Nafikiri wakati mwingine tunakuwa na haraka sana kuanza kulaumu kuwa hachezi, amefeli," alisema Solskjaer akinukuliwa na Sky Sport'. "Lakini Victor na Fred kama mfano, inachukua muda kidogo sasa wanakuwa wachezaji muhimu zaidi kikosini, itakuwa hivyo kwa Donny."

HABARI MICHEZO

# Guardiola amwaga sifa kwa Stones

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesema, John Stones amethibitisha kwamba yeye anafiti pale Manchester City baada ya ushindi dhidi ya Manchester United kwenye mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la EFL.

Stones alifunga bao lake la kwanza kwa City tangu Novemba, mwaka 2017 na Fernandinho akafunga lingine kwenye ushindi wa magoli 2-0 katika dimba la Old Trafford, Jumatano usiku na kutinga fainali ambapo sasa watacheza na Tottenham.


Mlinzi huyo amekuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu, na Guardiola hakusita kumsifia Stones, ambaye alionekana kama vile hana namba kwenye kikosi hicho.

"Alionyesha kiwango cha kuvutia kabisa, lakini jambo la muhimu ni kwamba anaweza kufanya kitu chochote ambacho alikuwa hawezi kukifanya , kucheza mechi nne, tano, sita mfululizo. Hilo ni muhimu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Aliweza kumdhibiti (Marcus) Rashford, ambaye amekuwa hatari na mwenye akili, na pasi zake kwa Joao (Cancelo) zilikuwa zimesimama.

"Wote kama timu, Fernandinho, nahodha wetu, walionyesha kiwango cha kuvutia. Aliusoma mchezo vizuri na kucheza kwa kiwango bora kabisa.

"Wachezaji wote (Ilkay) Gundogan, Raheem (Sterling), Phil (Foden)...timu yote ilifanya vizuri kwa ujumla."







# SHAQIRI KUBAKIZWA LIVERPOOL

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wanaripotiwa kuwa sasa hawataweza kumtema Xherdan Shaqiri kwenye dirisha hili dogo la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Nyota huyo raia wa Uswisi alikuwa anatarajiwa kuwa yupo mbioni kuondoka pale Anfield mwezi huu, baada ya kuwa na muda mchache wa kucheza kwa msimu wote, akiwa ameanza katika mechi mbili tu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa chanzo kimoja cha habari za michezo cha nchini Uswisi kilichonukuliwa na ESPN, Liverpool wanajiona kama wamebanwa na athari za corona na klabu haipo katika mazingira ya kumwacha aondoke kwa sasa.

Shaqiri anatarajiwa kuendelea kuwapo pale Merseyside msimu wote wa 2020-21 na huenda akapata fursa zaidi ya kucheza kwenye nusu hii ya pili ya msimu.

Hata hivyo, hakuna taarifa kubwa sana za uhamisho pale Liverpool, na kocha Jurgen Klopp wiki iliyopita alisema kuna asilimia kubwa zaidi kwamba hakuna mchezaji yeyote mpya kabla ya dirisha kufungwa Februari ambaye hatasaini.

# *Inter Miami yamtaka Neville*

**LOS ANGELES,** Marekani

INTER Miami wameripotiwa kuwa wamejaribu kufanya mawasiliano na kocha wa timu ya taifa ya Wanawake ya England, Neville kwa ajili ya kumpa kazi klabuni hapo.

Taarifa zinasema kuwa mazungumzo ya awali kati ya pande hizi mbili tayari yamefanyika.

David Beckham, ambaye ni mwanatimu mwezake wa zamani wa Neville kule Manchester United ni mmiliki mwenza wa klabu ya Inter Miami na pia ana umiliki wa aina hii kwa timu ya Ligi Daraja la pili ya Salford nchini England.


Neville anajiandaa kuacha kibarua chake kwenye timu ya taifa ya wanawake hapo Julai, mwaka huu ambapo ndiyo itakuwa tamati ya mkataba wake wa sasa.

Wakati huo huo, pale Inter Miami kumekuwa na sintofahamu juu ya hatima ya kocha wake wa sasa wa klabu hiyo, Diego Alonso.

Neville amekuwa kocha wa timu ya taifa ya wanawake ya England tangu Januari, mwaka 2018 na kwa nafasi yake aliweza kukiongoza kikosi hicho kufikia nusu fainali ya Kombe la Dunia la Wanawake mwaka 2019 kule Ufaransa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# VILLA YAMWEKA SOKONI GREALISH

## Yataja kiasi cha fedha wanachotakiwa United kulipa ili kunasa saini ya nyota huyo...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United wanahitaji kujiandaa tayari kutumia pauni milioni 90 kama wakihitaji kuinasa saini ya Jack Grealish kutoka Aston Villa, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Nyota huyu raia wa England bado anaendelea kuhusishwa na uhamisho wa kutijiunga na klabu hiyo Old Trafford licha ya United kuamua kumsajili, Donny van de Beek msimu wa majira ya joto uliopita.

**Grealish amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia pale Villa msimu huu, akiwa ametoa jumla ya asisti mbalimbali na kufunga magoli 15 kwa pamoja kwenye mechi zake 15 za Ligi Kuu England alizocheza msimu huu.**

Aston Villa wanatambua na kukubaliana na ukweli nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 atashawishiwa kwenda sehemu nyingine, lakini vyanzo vingine vinasema watahitaji kuruka kiunzi cha dau kubwa kuinasa saini yake.

Grealish alisaini mkataba mpya na Villa Septemba, mwaka jana, na mkataba wake wa sasa utashuhudia akiendelea kuitumikia klabu hiyo hadi mwisho wa msimu wa 2024-25, ikiwa hatakamilisha uhamisho wowote.

Paul Dybala kutoka Juventus pia anatajwa kuwa kwenye malengo ya United, hata hivyo, mpango huu wa kocha Ole Gunnar Solskjaer unaonekana kutokuwa na matumaini ya kufanikiwa katika dirisha hili la Januari.

## ZISIKUPITE

### MESSI NJIA MOJA

MGOMBEA urais wa Barcelona, Agusti Benedito, amesema hafikirii kama Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, ataongeza mkataba wake wa sasa, ambao unamalizika Juni mwakani. ***(Goal)***

### MESSI, CITY KITAELEWEKA

MANCHESTER City wanaamini wako mbele kwenye mbio za kumsajili, Lionel Messi kama raia huyo wa Argentina ataondoka Barcelona kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Telegraph - subscription required)***

### EVERTON KUMUUZA KEAN

EVERTON inatarajiwa kupokea ofa kwa ajili ya Moise Kean mwenye umri wa miaka 20, kutoka Paris St-Germain, ambako fowadi huyo wa timu ya taifa ya Italia anacheza sasa kwa mkopo. ***(Liverpool Echo)***

### OZIL HUYO FENERBAHCE

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, mwenye umri wa miaka 32, amekubali mkataba wa miaka mitatu na nusu na klabu ya Uturuki ya Fenerbahce. ***(DHA)***

### WIJNALDUM AKWAMA

MAZUNGUMZO kati ya Liverpool na kiungo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30 yamesimama. ***(Sky Sports)***

### SON, SPURS SAFI

KLABU ya Tottenham Hotspur imefikia makubaliana na fowadi wa Korea Kusini, Son Heung-min mwenye umri wa miaka 28, na atasaini mkataba mpya utakaomweka klabuni hapo kwa muda mrefu. ***(Telegraph - subscription required)***

### SNODGRASS SOKONI

KLABU ya West Brom imefikia hatua nzuri ya mazungumzo ya kumsajili winga wa Scotland, Robert Snodgrass mwenye umri wa miaka 33, kutoka West Ham. ***(Sky Sports)***

### RASHFORD GHALI DUNIANI

STRAIKA wa Manchester United na England, Marcus Rashford (23), ni mchezaji mwenye thamani kubwa zaidi duniani, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Taasisi ya CIES na anatajwa kuwa na thamani ya euro milioni 165. ***(CIES Football Observatory)***

### CUTRONE KURUDI WOLVES

KLABU ya Wolves inafikiria kumwita straika wa Timu ya Taifa ya Italia, Patrick Cutrone (23), kutoka Fiorentina anakocheza kwa mkopo ili kwenda kuziba pengo la Raul Jimenez ambaye ni majeruhi. ***(Mail)***

### TRAORE AGOMBEWA

WEST Ham na Wolves zinapambana kuwania saini ya mshambuliaji wa Ajax na Timu ya Taifa ya Burkina Faso mwenye umri wa miaka 19, Lassina Traore. ***(De Telegraaf, via Sun)***

HABARI MICHEZO

# Bonanza la Mati lafana Manyara

**Na Mwandishi Wetu,** MANYARA

TIMU ya Strong Coffee imeibuka kidedea baada ya kuichapa Strong Dry Gin mabao 2-0 katika mchezo wa fainali ya bonanza maalumu lililofanyika kwenye Uwanja wa Singe, Babati kwa lengo la kuuaga mwaka uliopita na kuukaribisha mwaka mpya wa 2021.

Bonanza hilo liliandaliwa na Kampuni ya Mati Super Brands na kushirikisha viongozi pamoja na wafanyakazi wote wa kampuni hiyo kutoka maeneo tofauti ya nchini.

Mabao katika mchezo huo yalifungwa na washambuliaji tegemeo wa timu hiyo ambao ni Johnson Mlay na Hassan Hamis.

Katika mchezo wa WAR, washindi walikuwa ni Strong Dry Gin wakati katika kukimbiza kuku upande wa wanaume aliyeshinda ni mfanyakazi wa kitengo cha Masoko, Kusiri na upande wa wanawake Meneja Burudani wa The Champions lounge, Teddy aliibuka kidedea.

Mathias Masele aling'ara katika shindano la kula, alishinda mfanyakazi katika kitengo cha masoko na mauzo mkoani Tanga, Mathias Masele.

Mapema katika ufunguzi wa bonaza hilo, Mkurugenzi, David Mulokozi, alisema lengo la bonanza hilo ni kudumisha umoja na ushirikiano miongoni mwao kuanza mwaka 2021 kwa furaha.

Mulokozi pia aliwashukuru wafanyakazi wa kampuni hiyo kuwaahidi wataendelea kufanya kazi kwa kufuata misingi na weledi katika kipindi cha mwaka huu.



Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo Brigedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo (aliyeshika chupa), akifurahia zawadi ya kinywaji cha Johnnie Walker baada ya Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), kutangaza udhamini wa mashindano ya mchezo huo yatakayofanyika hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi wa Masoko wa SBL, Mark Mugisha na Kepteni wa klabu hiyo, Japhet Masai (kushoto) na Minga Lumuli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MICHUANO YA JOHNNIE WALKER WAITARA YAIVA

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa gofu kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini wanatarajia kupambana katika mashindano ya Johnnie Walker Waitara ambayo yamepangwa kufanyika Januari 21, mwaka huu kwenye viwanja vya gofu vya Lugalo jijini Dar es Salaam.

**Mashindano hayo ya siku moja yameandaliwa na Klabu ya Gofu ya Lugalo na kudhaminiwa na kinywaji cha Johnnie Walker kinachosambazwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti na yanatarajia kuwashirikisha zaidi ya wanamichezo 150.**

Awali mashindano haya yenye mvuto wa aina yake na ambayo pia yatawaleta wachezaji gofu wa kulipwa, yalitarajiwa kufanyika mwezi uliopita.

Mwenyekiti wa klabu ya Lugalo Brigedia Jenerali mstaafu, Michael Luwongo, alisema maandalizi yote ya michuano hiyo yamekamilika na anawataka mashabiki wa mchezo huo kujitokeza siku ya mashindano.

"Tunayofuraha kuutangazia umma kuwa maandalizi ya mashindano yetu yapo katika hatua nzuri. Pia tunapenda kutoa shukrani zetu kwa wadhamini wetu Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia kinywaji cha Johnnie Walker ambao ndiyo wanawezesha mashindano haya makubwa kabisa hapa nchini kuweza kufanyika," alisema Jenerali Luwongo.

Alifafanua SBL imekuwa mdhamini mzuri kwenye mashindano hayo na kuongeza kuwa ni mdau mkubwa katika maendeleo ya michezo hapa nchini hususani mchezo wa gofu.

Mashindano ya Waitara hufanyika kila mwaka yakiwa na lengo kubwa kumwenzi Mkuu wa Majeshi mstaafu Generali George Waitara, kutokana na mchango wake kwa michezo ikiwa ni pamoja na kuanzisha michuano hiyo ambayo hufanyika katika viwanja vya Lugalo hapa jijini.

Meneja wa pombe kali wa SBL, Minga Lumuli alisema Johnnie Walker inajivunia kuwa mshirika katika mashindano hayo yenye heshima kubwa ndani na nje ya nchi na kuongeza kinywaji hicho kitaendelea kusaidia maendeleo ya michezo ikiwa ni pamoja na gofu.

Kwa mujibu wa Lumuli, mashindano hayo yamegongana na maadhimisho ya miaka 200 tangu kuanza kutengenezwa kwa Whisky hiyo maarufu duniani na kuongeza kuwa kinywaji hicho kinafurahia kuadhimisha mafanikio yake ya kipindi chote hicho kwa kuungana na wachezaji wa gofu kutoka sehemu mbalimbali nchini.

"Wakati tukisherehekea miaka 200 tangu kuanza kutengenezwa kwa JW ambayo kwa sasa ni wisky namba moja ulimwenguni, tunayofuraha kusafiri katika miaka yote hii tukiendelea kuwa imara na katika ubora ule ule," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya NIC, Dk. Elirehema Doriye (kushoto), akimkabidhi mkataba wa udhamini wa mbio za Goba Hills Marathon 2021, mratibu wa mbio hizo, Benson Luoga, jana, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIC yaibeba Goba Hills Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima ya NIC imetangaza kuwa mdhamini mkuu wa mbio za Goba Hills Marathon kwa msimu huu ambazo zimeandaliwa na klabu ya Goba Roads Runners (GRR) na zitafanyika Januari 31, mwaka huu kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Goba jijini Dar es Salaam.

Kauli mbiu ya mbio hizo mwaka huu ni "Kimbia, Okoa Maisha ya Mama na Mtoto" ambapo lengo kuu ni kuboresha afya ya mama na mtoto kwa kuboresha mazingira ya hospitali hasa wodi za kujifungulia za wanawake.

Hii ni mara ya pili kwa mbio hizo kufanyika baada ya mafanikio ya msimu wa kwanza wa mbio hizi uliyofanyika Februari, mwaka jana.

Akizungumza jijini jana, wakati wa kutangaza kudhamini mbio hizo, Mkurugenzi Mtendaji NIC, Dk. Elirehema Doriye, alisema kampuni yao inajivua kuwa mdhanini mkuu wa mbio hizo na mwaka huu watatoa kiasi cha Sh. milioni 25 kufanikisha mashindano hayo.

Dorye alisema michezo kwa siku hizi ni ajira na ili ajira ipitakane uwekezaji mkubwa unahitaji na anaamini udhamini wao utachangia kuzalisha wanariadha ambao wataiwakilisha nchi kwenye mashindano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Kiongozi huyo aliwakumbusha Watanzania kutaka bima kwenye michezo ni muhimu kwani pale mchezaji anapoumia na kuwa nje ya uwanja anahitaji kuendelea kuishi maisha yake ya kila siku na hivyo wao NIC wapo kwa ajili ya kutoa hitaji hilo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Goba Hills Marathon, Benson Luoga, alisema kuwa mbio hizo zitakuwa za kilomita 42.2, kilomita 21.1, kilomita 10 na za kilomita tano maarufu 'Family Run'.

Luoga alisema usajili kwa ajili ya kushiriki mbio hizo Sh. 30,000 na tayari usajili umeshafunguliwa na washiriki wameanza kujisajili kupitia tovuti ya klabu ambayo ni www.grr.co.tz.

# Michezo

Ijumaa Januari 8, 2021

Nipashe




Villa yamweka sokoni Grealish UKURASA 22



Beki wa Simba, Shomary Kapombe (kulia), akiruka juu ili kuondoka na mpira dhidi ya mchezaji wa FC Platinum katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba: Tumetekeleza

## Kocha ajivunia kiwango, yahamishia dozi Mapinduzi...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Mbelgiji, Sven Vandenbroeck, amewamwagia sifa wachezaji wake kwa kuonyesha kiwango cha juu katika mechi ya marudiano dhidi ya FC Platinum na kutinga hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kitendo hicho ni cha kupongezwa.

**Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba walisonga mbele katika mashindano yao ya kimataifa kwa jumla ya mabao 4-1.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kabla ya kikosi cha timu hiyo kwenda Visiwani Zanzibar, Sven alisema matokeo ya mechi hiyo yalikuwa mazuri na kilichomfurahisha ni baada ya wachezaji wake kufuata maelekezo aliyoyatoa wakiwa kwenye mazoezi.

Sven alisema mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa baada ya wapinzani wao kucheza kwa kuzuia katika dakika 45 za kipindi cha kwanza hali ambayo ilimpa wakati mgumu kwa 'Plan A' kutokana na muda mrefu wapinzani wao kukaa nyuma na kuwabana wachezaji wake kucheza soka lililozoeleka.

"Ilikuwa mechi ngumu na ushindani kwa sababu waliingia kwa kutaka kuzuia, ila wachezaji wangu walifuata maagizo niliyowapa na kila mmoja alionyesha kiwango kizuri na kufanikiwa kufuzu na kucheza hatua ya makundi ya michuano hiyo."

"Kulingana na jinsi ya wapinzani wetu walivyoingia, na sisi kupata matokeo hayo niwapongeze wachezaji wangu wamepambana kwa dakika 90 kutafuta kile kilichokuwa kikitarajiwa na kila mshabiki wa Simba," alisema Sven.

Kocha huyo alisema mbali na uwezo wa timu, pia alifurahishwa na kiwango cha mchezaji mmoja mmoja ambapo kila mmoja alifanya majukumu ipasavyo hasa katika kipindi cha pili ambacho FC Platinum waliingia kwa kubadilika na kutaka kutafuta bao. Aliongeza sasa kikosi chake kinajipanga kutumia mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa ajili ya maandalizi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye Beki wa Simba, Erasto Nyoni, alisema juzi wachezaji, benchi la ufundi pamoja na viongozi wa timu hiyo wameufananisha ushindi huo na salamu za mwaka mpya wa 2021.

"Kuhusu penalti ya kwanza kwenda kupiga ilikuwa ngumu lakini baada ya wachezaji wenzangu wote walitaka nipige, ikanipa ujasiri na kujiamini kwamba hii ni ishara nzuri kwetu ya kusonga mbele, hivyo tulijiamini na kwenda kufunga bao la kwanza," alisema Nyoni.

Wakati huo huo aliyekuwa Waziri wa Mazingira na Muungano, Januari Makamba alisema uamuzi wa viongozi kuungana 'mkono' linapokuja jambo ambalo linaleta manufaa ya nchi unasaidiwa timu shiriki kupata matokeo mazuri.

"Tuwapongeze Simba na Namungo FC, wameipeperusha vyema bendera ya Tanzania, inapofika jambo hilo basi hizi itikadi zetu za U-Yanga na U-Simba tuziweke pembeni na kutakiwa kuungana nao wawakilishi hao kupigania jambo la nchi, kama ilivyo sasa ushindi wa hizo timu zimeongeza pointi tatu, zitakazotusaidia mwakani kuingiza timu nne," alisema Januari.

Simba ilianza michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kucheza dhidi ya Plateau United ya Nigeria na ilisonga mbele kwa ushindi wa bao 1-0, walilolipata ugenini huku ikilazimishwa suluhu hapa nyumbani.

# Simba, Yanga kujiuliza Z'bar

**Na Adam Fungamwango**

MASHINDANO ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mapinduzi yanatarajiwa kuendelea tena leo kwa vigogo wa soka nchini kushuka dimbani kuwania pointi muhimu za michuano hiyo inayofanyika kila mwaka Visiwani Zanzibar.

Yanga iliyoanza kampeni ya kuwania taji hilo kwa kutoka suluhu dhidi ya Jamhuri, leo itavaana na Namungo FC jioni katika mechi yake ya mwisho ya hatua ya makundi wakati Simba inachuana na wenyeji Chipukizi kuanzia saa 2:15 usiku, mechi zote zilifanyika kwenye Uwanja wa Amaan.

Kikosi cha Cedric Kaze kinakutana na Namungo ambayo pia imesonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Hilal Obeid kwa ushindi wa jumla wa mabao 5-3.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kwa muda mrefu sasa hawajalitwaa kombe hilo, msimu huu wamepeleka kikosi kamili ambacho wanaamini kitapambana na hatimaye kufanya kile kinachotarajiwa na mashabiki wa timu hiyo.

Bumbuli alisema mchezaji wao ambaye amekuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wa timu hiyo, Saido Ntibazonkiza huenda akarejea tena uwanjani baada ya kutoonekana katika mechi ya kwanza kwa sababu ya kuwa majeruhi.

"Hatuangalii tulipojikwaa, na kocha ametambua upungufu wa mechi ya kwanza. Huenda leo akamtumia Saido aliyekuwa majeruhi kwa sababu tunahitaji kujiweka pazuri na kutinga hatua ya nusu fainali," alisema Bumbuli.

Naye Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema wako tayari na kamili kwa mchezo huo wa kwanza na kwake anaipa umuhimu mkubwa michuano hiyo.

Sven alisema wanaingia katika michuano hiyo wakiwa hawaidharau, na kuweka pembeni mafanikio waliyopata ya kutinga hatua ya makundi kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Sisi lengo letu ni kuchukua kila kombe katika mashindano ambayo tunashindania, hata hilo Kombe la Mapinduzi tunalihitaji pia," alisema kocha huyo.

9 770856 541002 >